

**Usajili** wa ndoa, talaka kufanyika kidigitali nchini

UKURASA 4

**Afariki** dunia kwa kukanyagwa na tembo kisa kelele

UKURASA 2



SAIF AL-ISLAM GADDAFI
Licha ya kuzushiwa kufa, yu hai akitamani urais
Ukurasa 14

Ukurasa 12
MWINYI Vs UONEVU ZANZIBAR

siasa
JUMATANO AGOSTI 11, 2021
Nipashe
HABARI BORA NA KAMILIFU

Ukurasa 12
TEHAMA inavyosaidia kupunguza gharama za ununuzi serikalini

KUKATAA CHANJO CORONA

• Polepole anapoonekana mpinzani

Na Sabato Kasika

WACHAMBUZI wa masuala ya kisiasa wanamtizama katibu wa zamani wa Itikadi na Uenezi wa CCM taifa, Humphry Polepole, kuhusu kile alichoandika kwenye mitandao ya kijamii kuikataa chanjo ya COVID-19. Wanaona kuwa anaweza kuwachanganya wananchi kwa vile ana wafuasi wengi ndani ya jamii. Lakini pia anachosema kinapinga maelekezo ya bosi wake na Mwenyekiti wa CCM.

Wakitoa maoni kufuatia andiko lake ambalo amelipa kichwa cha habari, Kalamu ya Humphrey Polepole, amezungumza mengi, akitaja msimamo wake kuwa kuishinda hofu ni silaha muhimu zaidi dhidi ya virusi vya corona.

Lakini, pia anaandika kuwa ni nyenzo muhimu ya kuimarisha uchumi na kuleta maendeleo kwa watu, huku akiipongeza seri-

Msonga, anasema, alichoandika mwanasisa huyo kwenye mitandao ya kijamii, ni sawa na kupingana na maelekezo ya serikali yanayotolewa na Rais na Mwenyekiti wa CCM Taifa, Rais Samia Suluhu Hassan.

"Ninasema anapingana na msimamo, kwa sababu tayari msimamo ulishatolewa kuwa chanjo ni hiari, sasa yeye alikuwa na sababu gani kuandika tena jambo hilo hilo? Inaweza kusababisha mpasuko," anasema Msonga.

Msonga anaona kuwa kilichoandikwa na Polepole ni tatizo tena ni kwenda kinyume na uwajibikaji wa pamoja, na kwamba kauli hiyo inaonyesha kuwa huenda kuna ajenda nyingine zaidi ambayo iko nyuma ya pazia.

katika ibara ya 18 ya katiba ya nchi yetu iwe ni kukubali au kupingana na serikali, kwani yeye ni mbunge tu siyo waziri," anakumbusha Mwakatobe.

Mchambuzi huyo wa siasa anasema, Polepole hajasema kinyume na kile ambacho serikali imeelekeza kuhusu chanjo kuwa ni hiari, na kwamba yeye ametumia uhuru kutoa msimamo wake kwa kueleza kuwa hatakwenda kuchanjwa.

" Watanzania hatuna utamaduni wa kukosoa serikali, ndiyo maana baadhi ya watu wanaamini kwamba amefanya kosa, lakini ametumia uhuru ambao umo ndani ya katiba kutoa maoni yake," anasema na kukumbusha kuwa kila mmoja ana haki ya maoni.

Anafafanua kuwa kinachoendelea sasa, ni mabishano kati ya wanaochanjwa na wasiochanjwa...

KURASA 11

Jumatano Agosti 11, 2021 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

# Nipashe

ISSN 0856 • Na. 0580669

www.ippmedia.com
www.twitter.com/nipashetz
www.facebook.com/nipashetz
www.instagram.com/th

# CHADEMA yatuma ujumbe kwa Samia



Katibu Mkuu wa CHADEMA, John Mnyika

Rais Samia Suluhu Hassan

UKURASA 2

UKURASA WA 7

## WAFIKISHWA MAHAKAMANI MADAI BIASHARA USAFIRISHAJI BINADAMU

RAIA wa Misri, Mohammed Shalabi na wenzake wawili, wamefikishwa katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu kwa tuhuma za usafirishaji haramu wa binadamu, wanadaiwa kuwasafirisha watu 95. Washtakiwa hao walipanda kizimbani mbele ya Hakimu Mkazi Mfawidhi, Godfrey Isaya, na kusomewa mashtaka na Wakili wa Serikali...



UKURASA WA 7

## MBARONI MADAI KUFANYA MATUKIO YA UHALIFU

JESHI la Polisi Mkoa wa Pwani linawashikilia watu 50 kwa tuhuma za kuhusika na matukio mbalimbali ya uhalifu wakiwamo wanane ambao ni wahamiaji haramu. Kamanda wa Polisi Mkoa wa Pwani, Wankyo Nyigesa, alisema...

# Kachero adai Sabaya alivamia duka na kuiba



**DAKTARI** : Msangi alipigwa, masikio yakavilia damu... *Endelea ukurasa 2& 3*

# Adaiwa kujinyonga baada ya kutoka jela

UKURASA 3

**MICHEZO** CHAMA, MUKOKO SHIDA NYINGINE SIMBA, YANGA UK. 24 **MAONI, KATUNI** UK.6

## Afariki dunia kwa kukanyagwa na tembo

**Na Lilian Lugakingira,** BUKOBA

MKAZI wa Kijiji cha Rugaze, Halmashauri ya Wilaya ya Bukoba, mkoani Kagera, Anajozia Chrisant (43), amepoteza maisha baada ya kukanyagwa na tembo.

Kamanda wa Polisi mkoani Kagera, Revocatus Malimi, alisema tukio hilo lilitokea Agosti 6, mwaka huu, saa nne usiku, baada ya kundi la tembo kuvamia kijiji hicho na kusababisha wananchi kupiga kulele za kuomba msaada.

Alisema siku ya tukio, mama huyo alikuwa na taarifa ya jirani yao kuwa mgonjwa na kutokana na kelele za wananchi hao alitoka nje ya nyumba akiwa peke yake kwenda kwa jirani yake anayeumwa, akidhani amefariki.

"Alipotoka nje alikutana na kundi la tembo ambao hawajafahamika idadi yao na pia haijafahamika walitoka hifadhi gani, mmoja wao alimshambulia kwa kumrusha juu na kisha kumkanyaga na kusababisha kifo chake papo hapo," alisema kamanda huyo.

Katika tukio lingine Jeshi la Polisi linamshikilia Violet Sylvester (25), mkazi wa Nyakahula, wilayani Biharamulo kwa mahojiano baada ya kushukiwa kuhusika na mauaji ya mzazi mwenzake Rashid Kasala (36).

Kamanda Malimi alisema watu hao waliokuwa wanandoa walizaa mtoto mmoja na kutengana zaidi ya mwaka mmoja uliopita, na kwamba wakati wakiwa na mahusiano walinunua kiwanja katika eneo la Nyakahula.

"Siku ya tukio Rashid alitoka Murgwanza kwenda Nyakahula na kufikia kwa mzazi mwenzake kwa lengo la kuuza kiwanja hicho, akitaka amsainie barua ya mauziano, na mwanamke huyo alitekeleza hilo, baada ya kuuza kiwanja hicho Rashid alibakia nyumbani kwa mzazi mwenzake huyo akisubiri wazungumze wamalize tofauti zao na kurudiana," alisema.

Alisema kabla ya kuuza kiwanja hicho kwa Sh. 800,000, baba huyo aliahidi kumpatia mzazi mwenzake Sh. 100,000 kutoka katika fedha atakazolipwa na mnunuzi, na baada ya kuuza alitekeleza ahadi yake hiyo.

Alisema wakati baba huyo akiendelea kusubiri, ilipofika saa tatu usiku, mama huyo alitoka nje kuzungumza na simu na wakati akiwa nje alisikia kelele za kuomba msaada na aliporudi aliona mtu akikimbia kutoka ndani ya chumba chake, lakini hakumtambua.

"Mama huyo anadai alipoingia ndani alikuta mzazi mwenzake akivuja damu nyingi baada ya kuchomwa na kitu chenye ncha kali sehemu mbalimbali za mwili wake, na kumpeleka kituo cha afya Nyakahula kwa kushirikiana na majirani, lakini alipoteza maisha wakati akiendelea kutibiwa," alisema Kamanda Malimi.

Alisema kufuatia mazingira ya kifo cha Rashid uchunguzi unaendelea ili kumbaini aliyeingia ndani ya chumba hicho na kumjeruhi kwa kitu chenye ncha kali, lakini wanamshikilia mama huyo kama mshukiwa namba moja kwa mahojiano.

# CHADEMA yatuma ujumbe kwa Samia

**Na Waandishi Wetu**

CHAMA cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) kimeiomba Ofisi ya Rais, Ikulu kupanga tarehe kwa ajili ya Rais kukutana na vyama vya siasa, kikisisitiza milango ya kuzungumza na Rais Samia Suluhu Hassan bado iko wazi.

Katibu Mkuu wa CHADEMA, John Mnyika, aliyasema hayo mkoani Dar es Salaam jana alipozungumza na waandishi wa habari kuhusu mambo mbalimbali yanayoendelea kisiasa nchini.

Mnyika alisema wakiondoa mambo waliyopanga kuzungumza na Rais katika kipindi cha kati ya mwaka 2016 na 2020, mbali na Uchaguzi Mkuu wa mwaka jana, pia kuna mambo mengi yamejitokeza yanayohitaji utatuzi wa uharaka.

"CHADEMA haijafunga milango ya mazungumzo na Rais, tupo tayari wakati wowote... ndiyo maana tumewaita kuzungumza katika hatua ya sasa kuwapa taarifa ya upande wetu yanayoendelea," alisema.

Mnyika alisema wanaamini Rais Samia atayasikia wanayosema na pale wasaidizi wake watakapompa taarifa za uongo, atachukua hatua.

Alisema hoja wanayoipigania ya kudai Katiba mpya ni kilio cha Watanzania na siyo vyama vya upinzani pekee.

"Tangu nchi ilipoingia kwenye mjadala wa kurejeshwa tena mfumo wa vyama vingi, ukiondoa maoni ya wananchi, upo ushahidi wa moja kwa moja wakati wa mchakato wa Katiba Mpya mwaka 2002 mpaka 2013, Tume ya Jaji Joseph Warioba ilipozunguka Tanzania Bara na Zanzibar, wananchi walieleza wanataka Katiba Mpya na iwe katiba ya wananchi," alisema.

Mnyika alisema nchi imeshatumia mabilioni ya shilingi kwenye mchakato wa Katiba Mpya, hivyo itakuwa hasara ukiendelea kukwamishwa.

Kuhusu zuio la mikutano ya hadhara nchini, Mnyika alisema wanaendelea kutafakari na muda ukifika wataweka bayana hatua wanazokusudia kuzichukua. Mnyika pia aligusia mahojiano ya Rais Samia na BBC, akibainisha kuwa tayari wamewaelekeza mawakili wanaomtetea Mwenyekiti wa CHADEMA, Freeman Mbowe, wachukue hatua za kisheria kuhusu kesi dhidi ya kiongozi wao huyo kutolewa kauli na viongozi nje ya mahakama.

Katika mahojiano yake na BBC, Rais Samia alisisitiza nia yake ya kukutana na viongozi wa vyama vya siasa nchini.

Rais Samia, alipozungumza na wahariri na waandishi wa habari waandamizi Ikulu jijini wakati wa maadhimisho ya Siku 100 za uongozi wake, alisema anakusudia kukutana na vyama vya siasa.

*Imeandaliwa na Romana Mallya na Haika Christopher, Sechellah Nakamba (SJMC) na Leyla Joho (TUDARCo)



Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Amos Mkala (wapili kushoto), akishuhudia utiaji saini wa mkataba kati ya Mratibu wa Barabara za Mitaa wa Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini (TARURA) wa mkoa huo, Mhandisi Geofrey Mkinga (kushoto), na mmiliki wa Kampuni ya Ujenzi ya Ibra Contractors, Mainda Waziri (kulia), jijini humo jana, ambapo kampuni nne zilitiliana saini mikataba ya ujenzi wa barabara mbalimbali za mkoa huo. Wapili kulia ni Mwanasheria wa TARURA, Bonaventure Mwambaja. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Kachero adai Sabaya alivamia duka, kuiba na kuteka nyara

**Na Allan Isack, ARUSHA**

ASKARI wa upelelezi, Konstable James (31), amedai mahakamani kwamba upelelezi uliofanywa na kikosi cha makachero, ulibaini kwamba aliyekuwa Mkuu wa Wilaya ya Hai, Lengai Ole Sabaya na wenzake, walivamia duka la Mohamed Saad, kupiga, kuteka nyara na kuwaweka chini ya ulinzi watu waliokuwa dukani hapo. Katika kesi hiyo ya jinai ya unyang'anyi wa kutumia silaha, mbali na Sabaya (34), wengine ni Sylvester Nyegu (26) na Daniel Mbura (38).

Hata hivyo, kabla ya kuanza kutoa ushahidi, washtakiwa walimkataa wakidai kwamba alikuwapo mahakamani akisikiliza ushahidi uliotolewa na mashahidi wengine lakini mahakama ilitupilia mbali madai hayo, hivyo kuendelea na ushahidi.

Akiongozwa na Wakili Mkuu wa Serikali Tumaini Kweka, alidai kwamba ni mpelelezi katika Ofisi ya Upelelezi Mkuu wa Upelelezi Wilaya ya Arusha (OC-CID) na katika majukumu yake kituoni hapo amefanya kazi kwa miaka 10.

James Alidai kwamba Februari 10, mwaka huu, mlalamikaji Bakari Msangi, alifungua jadala kituoni kuhusu tukio la shambulio la kudhuru mwili.

Konstebo James alidai kuwa alianza kazi hiyo majira ya saa 11 jioni akiwa ameambatana na OC-CID na makachero wengine pamoja na Numan Jasin kwenda kufanya upelelezi katika duka hilo.

"Nilimuuliza Numan kwamba maji yale yalitoka wapi akatueleza kwamba mmoja wa vijana waliokuwa dukani alijikojolea. Pia wakati tukikagua kutaka kupata uhalisia wa tukio hilo kwenye CCTV camera, tulibaini kamera nne 'footage' zilichezewa," alidai.

Pia alidai kwamba wakati wakimhoji Numan, aliwaeleza kwamba Sabaya na walinzi wake waliwashambulia kwa kuwapiga ngumi, mateke na vibao ndipo walibaini kwamba kuna kitendo cha kijinai kilifanyika dukani hapo.

"Katika ukachero wangu kamera hizo hazikuweza kutusaidia katika upelelezi wetu kwa sababu zilikuwa zimechezewa, hivyo tukatafuta ushahidi mwingine.

"Katika upelelezi wangu tulihoji mashuhuda wa tukio hilo na baada ya kuwahoji waliandika maelezo wakieleza Februari 9, mwaka huu, majira ya saa 11:00 jioni, walishuhudia magari tatu yakifika katika eneo la duka hilo na walishuka kwenye watu wapatao 10, akiwamo Mkuu wa Wilaya ya Hai, Lengai Ole Sabaya, na waliingia ndani na baadhi walibaki nje na mlango wa duka ulifungwa nusu.

"Mashuhuda hao walishudia baadhi watu watatu waliokuwa nje walikuwa wameshika bastola na bunduki kubwa," alidai.


Kadhalika, alidai kwamba Bakari Msangi alipokwenda Hospitali ya Mount Meru kutibiwa, alipigwa picha za mnato mtaalamu wao akiwa na majeraha na walizituma katika Kamisheni ya Uchunguzi wa Kisayansi (CFB), iliyoko Dar es Salaam kwa ajili ya upelelezi zaidi.

Alidai kwamba walipiga picha tano kama sehemu ya kukamilisha ushahidi na kuithibitishia mahakama kuwa mhanga huyo alipigwa na kushambuliwa.

Shahidi huyo aliwasilisha mahakamani picha tano za mnato na barua kutoka CFB, ikionyesha kwamba picha hizo zimefanyiwa kazi katika kamisheni hiyo.

"Baada ya kupokea majibu hayo nilihakiki picha kama ni zenyewe na niliziambatanisha katika jalada ya mashtaka," alidai.

HABARI KITAIFA



Mkurungenzi Mtendaji wa Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO), Dk. Tito Mwinuka (kushoto), akibadilishana mkataba wa awali wa upembuzi yakinifu wa uzalishaji wa umeme wa makaa ya mawe Kiwira na Kaimu Mkurungenzi wa Mtendaji wa Shirika la Madini la Taifa (STAMICO), Dk. Venance Mwasse jijini Dodoma jana.
**PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Adaiwa kujinyonga baada kutoka jela

**Na Said Hamdani, LINDI**

MKAZI wa Mtaa wa Nangando Halmashauri Wilaya ya Liwale mkoani Lindi, Faraji Likange (35), anadaiwa kufariki dunia kwa kujinyonga kwa kutumia kamba ya pazia kwa madai ya ugumu wa maisha ya uraiani baada kutoka jela.

Kwa mujibu wa taarifa za ndugu na majirani zilizothibitishwa na mamlaka husika za ulinzi na usalama ngazi ya mkoa, Likange aliondoka nyumbani kwao Agosti 3, mwaka huu na hakuonekana tena hadi Agosti 7, mwaka huu majira ya mchana mwili wake ulipokutwa unaning'inia kwenye mti eneo la makaburi.

Majirani hao wakiwamo Yusuf Juma, Kindamba Hemedi, Lucy Joseph na mama mzazi wa Likange, walidai kuwa mwili wake ulikutwa unaning'inia juu ya mti wa mkorosho eneo la makaburi ya Mtaa wa Nangando mjini Liwale ukiwa umeharibika.

"Baada ya kumtafuta takribani kwa siku nne, hatimaye tukaukuta mwili wa Faraji ukining'inia juu ya mti wa mkorosho.

"Wamesema kupatikana kwa mwili huo kulitokana na harufu iliyokuwa ikisikika ya kitu kilichooza kutoka eneo la makaburi yaliyopo Mtaa wa Nang'ando," alidai Juma.

Mashuhuda hao walisema kuwa kutokana na mwili kuharibika, mara tu baada ya kukamilika kwa uchunguzi wa wataalamu wa afya na Jeshi la Polisi, wananchi walichimba shimo usawa ulikokuwa unaning'nia mwili huo kisha wakakata kamba na kuufikia mwili huo.

Walidai kuwa Likange alirejea mjini Liwale mwishoni mwa mwaka jana, akitoka Gereza la Mtwara kutumikia kifungo kwa kosa la ubakaji.

Ilidaiwa kuwa baada ya kutoka gerezani, Likange alionekana mnyonge ya kutokuwa na furaha, akisikika akidai hali ya maisha ya uraiani kwa upande wake kutokuwa rafiki.

Mama wa Likange, Darini Ngambe, aliiambia Nipashe kuwa tangu kijana wake arejee nyumbani kutoka gerezani, hakuwa na furaha na mara nyingi alionekana mnyonge, akilalamika hali ugumu wa maisha uraiani.

Alidai kuwa wakati anaondoka nyumbani wiki iliyopita, hakumuaga mtu yeyote.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Lindi, Mtatiro Kitinkwi, akizungumzia tukio hilo, athibitisha kuwapo kutokea na kukiri kwamba Likange aliwahi kuhukumiwa kutumikia kifungo gerezani kwa kosa la ubakaji.

**"Wamesema kupatikana kwa mwili huo kulitokana na harufu iliyokuwa ikisikika ya kitu kilichooza kutoka eneo la makaburi yaliyopo Mtaa wa Nang'ando," alidai Juma.**

# Daktari adai alimpokea Msangi akiwa na uvimbe, damu imevilia

**Na Allan Isack, ARUSHA**

DAKTARI katika Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Arusha (Mount Meru), Ngiana Mtui (28), amepanda kizimbani kwenye Mahakama ya Hakimu Mkazi Mkoa wa Arusha kutoa ushahidi.

Amedai kuwa mahakamani huko kuwa alimpokea Bakari Msangi akiwa na hali mbaya na alikuwa na uvimbe wa damu masikioni na alama za majeraha ya kupigwa na kitu butu.

Shahidi huyo wa 10 wa Jamhuri alipanda kizimbani jana mahakamani huko kutoa ushahidi katika kesi ya jinai namba 105 yenye mashtaka matatu ya unyang'anyi wa kutumia silaha inayomkabili aliyekuwa Mkuu wa Wilaya ya Hai mkoani Kilimanjaro, Lengai Ole Sabaya (34) na wenzake wawili.

Akiongozwa na Wakili wa Serikali, Baraka Mgaya, shahidi huyo ambaye ni mkazi wa Kata ya Baraa, Halmashauri ya Jiji la Arusha, alidai amefanya kazi ya kitabibu Mount Meru kwa muda wa miaka miwili.

Daktari huyo alidai kuwa Februari 10 mwaka huu, akiwa kazini akiendelea na majukumu yake, majira ya usiku, alimpokea mgonjwa ambaye ni Bakari Msangi, akilalamika kuwa na maumivu makali sehemu za masikio, mashavu na usoni.

Shahidi huyo alidai ngozi ya mgonjwa huyo ilikuwa ikionyesha kuumia kwa kuwa ilikuwa na rangi nyekundu na alikuwa amevimba kwenye masikio na damu ilikuwa imeivilia ndani ya sikio.

"Mgonjwa alikuwa wa jinsia ya kiume, alikuwa na mchubuko na uvimbe kwenye sehemu za usoni, mashavuni na kwenye masikio na baada ya uchunguzi, tulibaini kwamba tukio hilo lilitokea kabla ya kufika hospitalini.

"Baada ya mgonjwa kufika hospitalini na kulalamika kwamba anahisi maumivu, tulianza kumpa huduma ya kwanza na kuendelea kumpatia matibabu kwenye sehemu alizodai kwamba amepata maumivu," alidai.

Shahidi hiyo alidai kuwa baada ya kupewa huduma za matibabu kwa kipindi kifupi, Msangi alimweleza kwamba maumivu yalipungua, hivyo hawakumlaza hospitalini, lakini walimpatia dawa na akaruhusiwa kwenda nyumbani.

"Tulipofanya uchunguzi, tulibaini kwamba mgonjwa alipigwa na kitu butu ambacho kilisababisha ngozi kubadilika rangi kuwa nyekundu na damu kuivia kwenye masikio na kitu kilichotumika hakikuwa cha ncha kali au kizito kwa kuwa kingemchana au kuvunja mifupa kwenye sehemu ambayo imeshambuliwa," alidai.

Daktari huyo alidai kuwa baada ya matibabu, walijaza fomu namba tatu ya polisi (PF3) na baada ya hapo walimruhusu mgonjwa kutoka hospitalini.

"Kwa utaratibu wa kawaida baada ya mgonjwa kupatiwa matibabu na PF3, kujazwa hapewi mgonjwa bali inahifadhiwa hadi hapo askari polisi watakapokuja kuifuata na sisi tunawakabidhi wao kwa ajili ya taratibu zingine," alidai.

Akihojiwa na Wakili wa Utetezi, Mosses Mahuna, shahidi huyo alidai kwamba Februari 10, mwaka huu, hospitalini huko alikabidhiwa PF3 na ndugu wa Msangi.

Wakili Mahuna alimhoji shahidi huyo kwa nini kwenye fomu ya PF3 imejazwa na kuonyesha mgonjwa alipigwa na watu 11 wakati daktari huyo hakuwapo eneo la tukio.

Katika majibu yake, shahidi huyo, alidai kuwa baada ya kumhoji mgonjwa (Msangi) ndipo alimweleza kwamba alipigwa na watu 11, hivyo aliandika maelezo hayo kwa kuyaingiza kwenye jalada la mgonjwa.

Vilevile, Wakili Mahuna pia alimhoji daktari huyo kwa nini fomu hiyo ya FP3 inaonyesha mgonjwa huyo alipelekwa hospitalini huko Februari 10 lakini fomu hiyo imejazwa Machi 10, mwaka huu.

Shahidi huyo alidai PF3 inajazwa siku ambayo polisi wanakwenda kuichukua hospitalini kama kuna kesi na fomu hiyo haijazwi siku ambayo mgonjwa amepelekwa hospitalini.

Mbali na Ole Sabaya, washtakiwa wengine wawili katika shauri hilo ni Sylvester Nyegu (26) na Daniel Mbura (38).


UBALOZI WA MAREKANI, DENMARK,
NORWAY NA HTT INFRACO LTD.
DAR ES SALAAM

## MNADA WA HADHARA:

**UNIVERSAL AUCTION CENTRE** Kwa idhini waliyopewa na Ubalozi wa **Marekani, Danish, Norway na HTT Infraco Ltd.** watauza kwa mnada wa hadhara Funicha za nyumbani, Generator,Pikipiki na Magari tarehe 14 August, 2021 Jumamosi kuanzia saa 4:00 asubuhi. Mnada utafanyika Golden Resort Sinza, Lion Street.

**Fenicha na Computer zitaanza kuuzwa kuanzia saa 4:00 asubuhi:** Sofa set, China base, Hutch, Chest drawer, Dresser, Credenza, Dining table, Conference table, Book case, Office desk, Chairs, Carpet, Vitanda, Magodoro, Fridge double door, Freezer, Ice maker, Washer, Dryer, Mashine za GYM, A/c split units, Mashine za Photocopy , TV set, Computer set, Laptop, Colour Printers, 7 Units Voltage Stabiliser 80 KVA, 2 Units Honda motorcycle CTX 200 na vingine vingi.

**Magari, Generator na Pikipiki yataanza kuuzwa kuanzia saa 6:00 mchana:**

| Idadi | Aind | Model | Mwaka | Ushuru |
|---|---|---|---|---|
| 3 | Nissan Hard body P/up Double Cabin | QD32 Diesel Engine | 2013 | Umelipwa |
| 1 | Nissan Hard body P/Up Single Cabin | QD32 Diesel Engine | 2013 | Haujalipwa |
| 3 | Suzuki Grand Vitara Station Wagon | J24B Petrol Engine | 2011/2012 | Umelipwa |
| 1 | Nissan X-Trail Station Wagon | NT32 Petrol Engine | 2014 | Haujalipwa |
| 1 | Suzuki Jimmy Station Wagon | M13A Petrol Engine | 2011 | Umelipwa |
| 1 | Nissan Almera Saloon | HR15 Petrol Engine | 2013 | Umelipwa |
| 1 | Generator 27 KVA Silence | Perkins Diesel Engine | - | Haujalipwa |
| 1 | Generator 12 KVA Silence | 4 Cylinder Diesel Engine | - | Umelipwa |

Mali zote zinaweza kukaguliwa Golden Resort Sinza,Lion Street kuanzia tarehe 11 mpaka 13 August, 2021, kuanzia saa 4:00 asubuhi mpaka saa 11:00 jioni.

**MASHARTI YA MNADA.**

1. Mnunuzi wa Fanicha atatakiwa kulipa malipo yote kwa keshia (cashier). Na mnunuzi wa Gari atatakiwa kulipa 25% pale pale na salio lilipwe ndani ya siku 4 za kazi mwisho wa kulipa tarehe 19 August, 2021 Saa 10:00 jioni. Ukishindwa kulipa kwa muda huo Gari au Generator litauzwa kwa mshindi mwingine aliyefata na dhamana haitarudishwa.
2. Malipo kwa njia ya **VISA na Master cards za CRDB na NBC** yanakubalika.
3. Mali zote zitauzwa kama zilivyo bila dhamana.
4. Mnunuzi atawajibika kulipa ushuru na kodi zingine zote.
5. Mali yote iliyouzwa itatakiwa kuondolewa baada ya kulipa malipo yote pamoja na kodi
6. Kila mtu atatakiwa lazima kuwa na bid namba itakayopatikana getini.
7. **Kila mtu anayesiriki mnada ni lazima kuvaa Barakoa na kunawa na maji tiririka au Sanitaiza Umbali wa mtu na mtu uzingatiwe.**

Kwa maelezo zaidi waone:
UNIVERSAL AUCTION CENTRE
PLOT NO: 5 "E" LION STREET SINZA
CELL NO: 0754 284 926
Insta: universalauctioncentre

DAR ES SALAAM
E-mail: universalauction@hotmail.com

116401502

# Usajili ndoa, talaka kufanyika kidigitali

**Na Mary Geofrey**

WAZIRI wa Katiba na Sheria, Prof. Palamagamba Kabudi, amesema Wakala wa Ufilisi na Udhamini (RITA) unaanzisha mfumo wa usajili wa ndoa kwa njia ya mtandao ambao utawezesha upatikanaji wa idadi ya ndoa zote zilizofungwa nchini.

Prof. Kabudi alibainisha hayo jana jijini Dar es Salaam wakati wa maadhimisho ya nne ya usajili wa matukio muhimu ya binadamu yaliyoandaliwa na RITA na kusema mfumo huo utasaidia kutoa nakala mtandaoni kabla ya nakala ya cheti cha ndoa kutolewa.

"Kabla mfumo huu haujaanza kufanya kazi, wadau wote waitwe wapewe elimu ya pamoja ya namna ya kwenda na teknolojia hii," aliagiza Prof. Kabudi.

Alisema rejista inawahusisha wanaofungisha ndoa kwa sababu siyo kila mtu ana mamlaka ya kufungisha ndoa kwa mujibu wa katiba ya nchi.

"Kiongozi wa ndoa ambaye hajasajiliwa kufungisha ndoa, akifungisha hiyo ndoa ni batili. Wenye ruhusa tu ndio wafungishe. Ambao hawana mamlaka watume maombi RITA wapewe kibali cha kufungisha ndoa," alisema Prof. Kabudi.

Alisema viongozi wengine wa dini ambao hawajasajiliwa wanaona kama ni usumbufu kufuata taratibu za kupatiwa kibali, lakini ni muhimu kwa ustawi wa taifa.

"Ndoa ni suala la hiari lakini kuvunjika kwake lazima serikali ihusike katika kuuvunja mkataba huo na wanaofungisha lazima nao wawe na kibali cha kufanya hivyo, siyo tu kila anayeongoza ibada anaweza kufungisha ndoa," alisema Prof. Kabudi.

Alisema duniani kote suala hilo linasimamiwa kikamilifu kwa sababu ndio msingi wa familia inayozalisha raia wa nchi husika.

Sambamba na hilo, aliwataka RITA kuhakikisha wanaendelea na jitihada za kusajili watoto chini ya miaka mitano kwa njia ya mtandao.

Alisema usajili wa watoto hao umefika katika mikoa 20 na jumla ya watoto milioni 6.5, sawa na asilimia 55 wamesajiliwa toka asilimia 13 ya mwaka 2012.

Kaimu Mkurugenzi wa Haki za Kisheria wa RITA, Lina Msanga, alisema watahakikisha wanasogeza vituo vya matumizi ya teknolojia karibu ili watoto chini ya miaka mitano wapate hati za kuzaliwa kwa kutumia simu za mkononi.

Alisema malengo yao ni kuhakikisha wanaongeza mwamko wa kusajili vifo, ndoa, talaka na sababu za vifo.

Maadhimisho hayo yalifanyika sambamba na semina ya viongozi wa kitaifa wa vyama vya watu wenye ulemavu.

# NCCR yashangazwa corona kupuuzwa

**Na Maulid Mmbaga**

CHAMA cha NCCR-Mageuzi kimedai serikali inalega katika kusimamia wananchi kuchukua tahadhari dhidi ya UVIKO-19, huku kikisema maelekezo ya kiafya yanayotolewa hayazingatiwi.

Naibu Katibu Mkuu wa NCCR-Mageuzi Bara, Anthony Calist, alibainisha hayo alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari jana jijini Dar es Salaam, na kwamba Mkuu wa Mkoa huo, Amos Makalla, amekuwa akitoa maelekezo ya uvaaji wa barakoa katika mikusanyiko na daladala kubeba 'level seat' lakini suala hilo limepuuzwa.

Alisema utafiti waliofanya wamebaini kwamba maelekezo ya serikali juu ya hadhari za ugonjwa huo yamepuuzwa na hayafuatwi hata kwa asilimia tano, huku akisisitiza watu kupata chanjo kwa kuwa viongozi wa NCCR-Mageuzi wakiongozwa na mwenyekiti wao, James Mbatia (pichani), wamepata na hadi sasa wako salama.



"Suala la UVIKO-19 kwetu ni ajenda ya kudumu, kwa sababu hali katika nchi yetu bado ni tete watu wanaendelea kupoteza maisha na kwa bahati mbaya sehemu kubwa ya umma wa Watanzania hatujaamka," alisema na kuendelea:

"Hatujaona hatari ambayo inatukabili, kwa upande wa pili sisi kama NCCR tunaona bado kuna ulegevu mkubwa katika yale ambayo kidunia yanatakiwa kufanywa."

"Tumesikia mkuu wa mkoa akitoa maelekezo kuwa magari ya umma yawe na 'level seat' na uvaaji wa barakoa, lakini mkichunguza mtabaini kwamba hayo maelekezo hayatekelezwi... kwenye mabasi watu wanarundikana kama kawaida, hatujui viongozi wanaishi sehemu nyingine na wananchi wanaishi kwingine, hivyo hawajui wananchi wanayoyafanya," alisema Calist.

Aliongeza kuwa maandalizi ya kukabiliana na janga la UVIKO-19 ni duni, kwani hospitali nyingi nchini zimeelemewa, na namna watu wanavyolichukulia jambo hilo wanaona kama ni suala la kawaida wakati hilo ni janga linalotakiwa kuchukuliwa hatua za makusudi ili kukabiliana nalo.


GSP AUCTION MART

P.o.Box 31088 Dar es Salaam Tanzania, Tel: + 255 687 638679 +255 654 922892 Sinza Africasana near by sokoni Africasana Block No. 31 Email: gsp.recovering@gmail.com / gsp.recovering@outlook.com

GSP AUCTION MART

**KUMB No. AFCL/2021/DM/026**

**GSP AUCTION MART** Kwa idhini na mamlaka tuliyopewa na kampuni ya **ALLIANCE FINANCE CORPORATION LIMITED** S.L. P 40780 Dar es salaam, tunapenda kutangaza mnada wa hadhara wa kuuza Magari kwa njia ya mnada wa magari twaja hapo chini.Siku ya Jumatano ya tarehe 18/08/2021 na siku ya Ijumaa ya tarehe 27/08/2021. Mnada utaanza Saa 5:00 kamili asubuhi katika yadi ya ALLIANCE FINANCE CORPORATION LIMITED iliyopo Dar es salaam vingunguti, Mwanza Sinai Mabatini na Arusha.

| CUSTOMER NAME | MODEL | VEH_NO | LOCATION |
|---|---|---|---|
| MOSES PETER ABDONI | LP 909 BUS | T877 DNN | DAR ES SALAAM |
| ABDALLAH KIBWANA KIBWANA | LP 909 BUS | T351 DPS | MWANZA |
| FILGONA RANGA DUKO | LP 909 BUS | T178 DPE | DAR ES SALAAM |
| LUKE ASSOCIATE LTD | PRIMA 2523 | T678 DNE | DAR ES SALAAM |
| LUKE ASSOCIATE LTD | PRIMA 2523 | T613 DMQ | DAR ES SALAAM |
| MAHENDA SOGONI CONSTRUCTION CO. LTD | LPK 2518 TIPPER | T264 DNX | DAR ES SALAAM |
| ROSEMARY GERVAS FILIPO | LP 909 BUS | T925 DQF | ARUSHA |
| MICHAEL WILLIAM KILIWA | LPT 1116 | T533 DSP | DAR ES SALAAM |
| MAGAMBO SAMWEL KISABO | LP 909 BUS | T334 DUF | MWANZA |

1. Dhamana itauzwa Kama ilivyo.
2. Mnunuzi anatakiwa kulipa siku hiyo hiyo ya mnada asilimia 25% ya bei iliyofikiwa.
3. Malipo ya asilimia 75% yalipwe ndani ya siku kumi na nne (14) kukamilisha malipo yote ukishindwa kufanya hivyo mnunuzi atakuwa amepoteza malipo yote ya awali ya asilimia 25% na mnada utarudiwa tena.
4. Gharama za kuona, kukaguwa, kuhamisha umiliki ni juu ya mnunuzi.
5. Kwa yeyote atakayeharibu mnada hatua kali za kisheria zitachukuliwa dhidi yake.

KWA TAARIFA ZAIDI WASILIANA NA:
GSP AUCTION MART PO BOX 310088 DAE ES SALAAM.
+255 654 922 892, +255 687 638 679

116402902


## Utafiti mchikichi waleta mafanikio

**Na Ashton Balaigwa, KIGOMA**

JITIHADA za Utafiti wa mbegu bora ya kisasa ya michikichi aina ya Tenera zilizofanywa na Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania (TARI) zimeanza kuonyesha matokeo chanya.

Hatua hiyo inatokana na mche wa mbegu hiyo, uliopandwa na Waziri Mkuu Kassim Majaliwa, kuanza uzalishaji kwenye kitalu kilichoko mkoani Kigoma.

Mche huo umeboreshwa kwa kuchanganya mbegu aina ya Dula inayotumiwa na wakulima wengi nchini na Pesifera na kuzalishwa kwa mbegu ya kisasa ya Tenera.

Baada ya utafiti huo, mbegu hiyo ilipandwa na Waziri Mkuu Majaliwa mwaka 2019 wakati wa uzinduzi wa upandaji mbegu bora ya mchikichi uliofanyika katika kitalu cha Gereza la Kwitanga.

Akizungumza katika ziara ya kujionea maendeleo ya michikichi ikiwa ni utekelezaji wa agizo la Waziri Mkuu, Mkurugenzi Mkuu wa TARI, Dk. Geofrey Mkamilo, alisema matokeo hayo chanya yamepatikana kabla ya miaka mitatu, muda uliokadiriwa kuanza uzalishaji.

"Waziri Mkuu alikuja kuzindua mche bora wa kisasa aina ya tenera mwaka 2019 na katika utafiti uliofanywa ulipaswa kuanza uzalishaji katika kipindi cha miaka mitatu tangu kupandwa lakini ndani ya miaka miwili tayari umeshazaa, haya ni mafanikio makubwa sana katika utafiti tuliofanya wa mbegu bora hii ya mchikichi aina ya tenera "alisema.

Dk. Mkamilo alisema mbegu hizo za kisasa aina ya Tenera zimegawiwa bure na serikali kwa wakulima wa mchikichi katika Mkoa wa Kigoma ili kuendeleza zao hilo kusaidia kuzalisha mafuta ya kula baada ya kufanyiwa utafiti kupitia kituo cha TARI – Kihinga mkoani hapa.

Alisema waliamua kufanya utafiti wa kuleta mbegu hiyo bora inayotumia muda wa miaka mitatu kuanza uzalishaji wa michikichi ili kuwasaidia wakulima kuacha kutumia mbegu ya muda mrefu ya Dula inayoanza uzalishaji baada ya miaka saba tangu ipandwe.

"Mbegu ya Tenera inatoa wastani wa tani tano mpaka sita za mafuta ya kula kwa hekta moja na ile ya zamani aina ya Dula inayotumiwa na wakulima wengi inatoa tani 1.5 kwa hekta. Kutokana na ongezeko hilo upatikanaji wa mafuta ya kula utakuwa mwingi katika kipindi kifupi," alisema Dk. Mkamilo.

Pia alisema Wizara ya Kilimo imekuwa ikifanya mikakati mbalimbali kuhakikisha inamaliza tatizo la mafuta ya kula nchini ambayo yamekuwa yakiagizwa nje ya nchi takribani tani 200,000 kwa kuongeza uzalishaji wa mazao ya mafuta kama michikichi, alizeti, nazi na kalanga.

Naye Kaimu Mkuu wa Gereza la Kwitanga, Bosco Mgema, alisema wameitikia agizo la Waziri Mkuu kwa kupanda mpaka sasa ekari 475 za michikichi aina tenera kwa ajili ya kuzalisha mafuta ya kula ambayo yamekuwa yakitumika katika Magereza mbalimbali na mengine kuuzwa.

Alisema kuwa uwekezaji huo wa kupanda Michikichi, utaenda sambamba na uanzishwaji wa kiwanda cha kukamulia mafuta ya kula na sabuni kupitia zao ambapo kwa sasa wameamua kuongeza uzalishaji.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Mapatano yalindwe SUK idumu Zanzibar

**BAADA** ya kumalizika kwa Uchaguzi Mkuu wa Zanzibar wa mwaka 2020 vyama vya siasa vya CCM na ACT-Wazalendo viliafikiana kuundwa kwa Serikali ya Umoja wa Kitaifa (SUK).

Kuundwa kwa serikali hiyo kulifikiwa baada ya kuwapo kwa mgogoro wa kisiasa uliotokana na uchaguzi huo, hivyo pande husika zikaona umuhimu wa kufanya hiyo ili kudumisha amani, mshikamano, umoja na maridhiano miongoni mwa Wazanzibari.

Katika makubaliano hayo, aliyekuwa Mwenyekiti wa ACT-Wazalendo ambaye alikuwa mgombea urais wake, Hayati Maalim Seif Sharif Hamad, alijumuishwa katika SUK na Rais Hussein Mwinyi, kwa kumteua kuwa Makamu wa Kwanza wa Rais.

Itakumbukwa kwamba hiyo haikuwa mara ya kwanza kuwapo kwa SUK Zanzibar. Mara ya kwanza iliundwa mwaka 2010 baada ya Katiba ya Zanzibar kufanyiwa marekebisho, hufuatia mazungumzo kati ya aliyekuwa Rais wa Zanzibar, Amani Abeid Karume na aliyekuwa Katibu Mkuu wa CUf, Hayati Maalim Seif Shaarif Hamad. Pamoja na nia njema na uzalendo ulioonyeshwa na Rais Mwinyi kurejesha SUK, hivi karibuni zimeonekana dalili ambazo zinatishia uhai wa serikali hiyo.

Baadhi ya matukio yaliyotokea kwenye uchaguzi mdogo wa ubunge Jimbo la Konde kisiwani Pemba wa Julai mwaka huu yametia doa uhai wa SUK, kutokana na viongozi wa ACT-Wazalendo kuyalalamikia kuwa yaliutia dosari uchaguzi huo.

Tusingetaka kuyarejea mambo yanayolalamikiwa, lakini viongozi wa ACT-Wazalendo wametoa masharti ya kushiriki tena kwenye uchaguzi huo, baada ya mshindi katika uchaguzi unaolalamikiwa kupitia CCM kutangaza kujiuzulu.

Juzi viongozi wa chama hicho cha upinzani wakiwa katika ziara kisiwani Pemba walisema hakitashiriki uchaguzi mdogo wa Jimbo la Konde hadi watumishi wa Tume ya Uchaguzi Zanzibar (ZEC), waliohusika katika uchaguzi uliopita watakapowajibishwa.

Kiongozi Mkuu wa Chama hicho, Zitto Kabwe, akisoma maazimio, alisema chama hicho hakitashiriki uchaguzi huo hadi watumishi wa ZEC wawajibishwe. ACT inasema wananchi ambao waliumizwa na kuteswa kwenye uchaguzi walipwe fidia, ili wapate haki yao. Pia inataka kuundwa kwa kamati ya kisheria ya kuratibu maridhiano ya kijamii, ili ZEC ionyeshe mwelekeo nini kifanyike ili maridhiano yazidi kukua. Pia kuitaka Serikali ya Zanzibar na ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuzifanyia marekebisho sheria zote za uchaguzi kabla ya mwaka 2025, ili uchaguzi mkuu ujao uwe sawa katika kushindania nafasi za uongozi.


Hata hivyo, kwa kuona athari zinazoweza kuhatarisha uhai wa SUK, baadhi ya hatua zimechukuliwa kuinusuru kama alivyoeleza Mjumbe wa Kamati Kuu ya ACT ambaye pia ni Makamu wa Kwanza wa Rais Zanzibar, Othman Masoud Othman, kwamba kilichomfanya mbunge mteule wa Konde kutoka CCM kuachia ngazi ni mazungumzo.

Kutokana na matukio kadhaa ambayo yaliwahi kutokea Zanzibar na kutishia umoja wa Wazanzibari, tunaona kwamba kuna kila sababu kwa viongozi wenye mamlaka pamoja na vyama vya siasa vinavyoinda SUK kuchukua hatua ili kuinusuru.

Jambo la msingi ni kuweka utaratibu mzuri wa mawasiliano na majadiliano ya kila mara husussan pale inapoonekana kuna mambo au matukio unayoweza kuleta mgawanyiko.

Tusingependa kuona matukio ya nyuma, yakiwamo yaliyovunja SUK ya mwanzo yakijirudia, hivyo tunawasihi waliopewa dhama kutanguliza mbele maslahi ya vyama na Zanzibar badala ya maslahi ya kwao binafsi.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Sabato Kasika

# Kuondoka corona kwa abiria, serikali iruhusu magari binafsi

**ILI** kupunguza msongamano wa abiria kwenye magari hasa daladala kwenye miji midogo na mikubwa, serikali inakumbushwa kutoa vibali kwa magari binafsi yaliyotayari kubeba abiria mijini ili kupunguza msongamano unaoweza kusababisha kuambukizana corona.

Ombi hilo linatolewa na Katibu Mtendaji wa Baraza la Ushauri la Utumiaji wa Usafiri wa Ardhi (LATRA-CCC), Leo Ngowi, baada ya kuona baadhi ya daladala na abiria hawazingatii mwongozo wa kudhibiti ugonjwa kwa kupandisha abiria kwa idadi ya viti maarufu kama 'seat level.'

LATRA-CCC inasema, kuna umuhimu wa kuongeza magari ya abiria ili huduma hiyo iwe rahisi katika kipindi hiki cha kujikinga na maambukizi ya Uviko-19, huku Jeshi la Polisi likiombwa kuwa makini na daladala zitakazoonyesha utovu wa nidhamu wa kuendelea kubeba abiria kupita kiasi tena ambao hawajavaa barakoa.

Inatoa ombi hilo baada ya kubaini kuwa tangu serikali itoe mwongozo wa kudhibiti ugonjwa huo, bado daladala za Dar es Salaam na kwenye miji mikubwa kuendelea kujaza abiria, licha ya kutakiwa kuzingatia 'level seat'.

Hiyo ndiyo hali halisi kwa daladala nyingi za jijini Dar es Salaam, hivyo ingekuwa jambo jema iwapo ombi hilo la LATRA-CCC kwa serikali litafanyiwa kazi haraka, ili kuepusha Watanzania kuambukizana corona.

Iwe kama mwaka jana, ambapo vibali vilitolewa haraka kwa baadhi ya magari yaliyosaidiana na daladala kusafirisha abiria kwenda na kurudi kwenye shughuli zao katika maeneo mbalimbali ya Dar es Salaam bila msongamano.

Katika mahojiano na wanahabari, anakumbushia kuwa wakati wa mlipuko wa kwanza wa corona, serikali ilitoa usajili mfupi wa magari 400 kwa ajili ya kubeba abiria kipindi cha asubuhi na jioni.

Kimsingi, hatua hiyo inaweza kumaliza tatizo hilo, kutokana na kwamba, daladala hazitoshi, hali inayosababisha abiria kulazimika kujazana na kusongamana bila kujali kuwapo kwa tishio la ugonjwa huo.

Ingawa wapo baadhi ya makondakta na madereva wanaolazimisha kujaza abiria, lakini magari yakiwa mengi hawatawapata kama ilivyo sasa, kwani watagawanyika kulingana na wingi wa magari.

Serikali imeshatoa maelekezo mengi kuhusu ubebaji wa abiria ndani ya daladala, huku Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Mkoa wa Dar es Salaam ikiwataka wamiliki wa vyombo vya usafiri kuwaelekeza madereva na makondakta kuuzingatia umuhimu wa kubeba abiria kwa idadi ya viti.

Maelekezo ya kamati hiyo ni baada ya kubaini kuwapo kwa ulegevu wa usimamizi katika baadhi ya maeneo, huku polisi, wakuu wa wilaya na LATRA, wakitakiwa kusimamia ipasavyo mwongozo wa serikali.

Pamoja na hayo, ninadhani kwamba, suluhisho la kero hiyo ni serikali kutoa vibali vya muda kwa magari binafsi kubeba abiria, kwani inaonekana njia nyingine zimekuwa ngumu kuleta matokeo chanya.

Ingawa daladala zinatakiwa kuepuka ubebaji abiria wasiovaa barakoa na hata kuwajaza kupita kiasi na kubeba wanafunzi watano watakaosimama, huku wakiwa wamevaa barakoa, hali halisi sivyo ilivyo.

Kwa hali ilivyo, ni kama wahusika wameshindwa kutekeleza maelekezo hayo yote, hivyo ingekuwa vyema kama vingetolewa vibali vya magari binafsi kama njia mbadala ya kukabiliana na corona kwenye usafiri.

Lakini pia chanzo cha kushindwa kutekeleza maelekezo hayo kinaweza kuwa ni uhaba wa daladala, lakini kama magari yataongezwa na bado abiria wanaendeleza kurundikana bila kuzingatia 'level seat', nadhani kutakuwa na sababu nyingine zinazotakiwa kufuatiliwa.

Hivyo, kuwapo kwa maelekezo ya idadi ya abiria kwa idadi ya viti bila mbadala wa kusaidiana na daladala, hali hiyo inaweza kuwa ngumu na kusababisha wengine kuchelewa kufika kazini au kurudi nyumbani kutoka kwenye shughuli za kuzalisha mali.

HABARI KITAIFA

# Wafikishwa mahakamani madai biashara usafirishaji binadamu

**Na Kulwa Mzee na Hadija Kitwana**

RAIA wa Misri, Mohammed Shalabi na wenzake wawili, wamefikishwa katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu kwa tuhuma za usafirishaji haramu wa binadamu, wanadaiwa kuwasafirisha watu 95.

Washtakiwa hao walipanda kizimbani mbele ya Hakimu Mkazi Mfawidhi, Godfrey Isaya, na kusomewa mashtaka na Wakili wa Serikali, Godfrey Ngwijo.

Ngwijo aliwataja washtakiwa wengine kuwa ni Ally Rajabu raia wa Tanzania na Chebet Benson raia wa Uganda.

Alidai washtakiwa wanakabiliwa na mashtaka matatu. Shtaka la kwanza, mshtakiwa wa kwanza, Mohammed anadaiwa kufanya biashara ya usafirishaji haramu wa binadamu.

Tukio hilo linadaiwa kutokea Agosti 4, mwaka huu, katika makazi ya Avon wilayani Ilala, akiwa raia wa Misri na Mauritania alikutwa akisafirisha watu 95, wakiwamo 90 Watanzania na watano raia wa Burundi.

Wakili Ngwijo akisoma shtaka la pili, alidai Ally anadaiwa kuandaa mpango wa kusafirisha binadamu.

Anadaiwa alifanya tukio hilo maeneo mbalimbali na Dar es Salaam, alikutwa akiandaa mpango wa kuwasafirisha watu hao ambao waliwapatia mafunzo kwa lengo la kuwapeleka katika nchi hizo.

Shtaka la tatu, mshtakiwa Chebet anadaiwa kufanya kazi nchini bila vibali kwamba katika Hospitali ya Kimataifa ya Sali iliyoko Masaki, Dar es Salaam.

Wakili Ngwijo alidai upelelezi dhidi ya Mohammed na Chebet umekamilika, hivyo aliomba tarehe ya kuwasomea maelezo ya awali wakati mshtakiwa Rajabu alikiri makosa yake.

Mohammed aliieleza Mahakama kwamba alikuja kwa mwaliko wa Rahma kwa lengo la biashara ndogo, alipofika aliuliza masuala ya vibali, alitakiwa kulipa Dola za Marekani 2,500 ili apate na alilipa. Mwanamke huyo anadai hana ofisi, alikamatwa akiwa nyumbani kwake. Hakimu Isaya alimwambia amewelewa wakati utafika wa kueleza hayo lakini kwa sasa si muda sahihi.

Mahakama ilikubali kuwapa dhamana kwa masharti ya kuwa wadhamini wawili wanaotambulika, mmoja mwajiriwa wa ofisi yoyote inayotambulika, kwa washtakiwa Mohammed na Chebet wanatakiwa kuwa na wadhamini watatu, wasalimishe hati zao za kusafiria na hawataruhusiwa kutoka nje ya Dar es Salaam bila ruhusa.

Kesi hiyo iliahirishwa hadi leo kwa ajili ya kuwasomea washtakiwa maelezo ya awali.

# 50 mbaroni madai kufanya matukio tofauti ya uhalifu

**Na Julieth Mkireri,**
KIBAHA

JESHI la Polisi Mkoa wa Pwani linawashikilia watu 50 kwa tuhuma za kuhusika na matukio mbalimbali ya uhalifu wakiwamo wanane ambao ni wahamiaji haramu.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Pwani, Wankyo Nyigesa, alisema jana kuwa watuhumiwa hao walikamatwa katika operesheni iliyoendeshwa na jeshi hilo kuanzia Julai 31, mwaka huu hadi juzi.

Alisema kati ya wahamiaji haramu waliokamatwa wawili ni raia wa Ethiophia na sita ni raia wa Bangladesh.

Wankyo alisema mbali na watuhumiwa hao, polisi pia wamekamata vitu vya wizi vikiwamo televisheni mbili, radio mbili, lita 380 za mafuta ya transfoma na bonaza tatu (dubwi) Vitu vingine vilivyokamatwa kwenye oparesheni hiyo, kwa mujibu wa Kamanda Wankyo ni pombe ya moshi lita 15, bangi puli sita, misokoto 12 na kete 315.

Pia alisema jeshi hilo limemkamata Sijali Iddi mkazi wa Miono wilayani Bagamoyo kwa tuhuma za kumiliki silaha aina ya gobore kinyume cha sheria.

Kamanda Wankyo alisema mtuhumiwa huyo alikamatwa Agost 4, mwaka huu, majira ya saa 11:00 jioni huko Msimbani kata ya Miono akiwa na gobore hilo, unga wa baruti na goroli 11 zinazotumika katika gobore.

Wankyo alisema uchunguzi unaendelea kuhusiana na tukio hilo na baada ya upelelezi kukamilika, mtuhumiwa huyo na wote waliokamatwa watafikishwa mahakamani kwa taratibu za kisheria.


**CHAMA CHA WAFANYAKAZI WA SERIKALI ZA MITAA TANZANIA (TALGWU)**

**TANGAZO LA MKUTANO MKUU WA TAIFA 2021**

Chama cha Wafanyakazi wa Serikali za Mitaa Tanzania (TALGWU) kinatarajia kufanya Mkutano Mkuu Taifa tarehe 24 – 25 Agosti 2021 katika ukumbi wa Mikutano wa Chuo cha Mipango Jijini Dodoma kuanzia saa 03:00 Asubuhi.

Agenda za Mkutano Mkuu Taifa zitakuwa ni kama ifuatavyo:

1. Kufungua Mkutano Mkuu
2. Kuthibitisha Agenda
3. Kusoma na kuthibitisha muhtasari wa Mkutano Mkuu wa tarehe 17 - 19 Desemba 2019
4. Yatokanayo na Mkutano Mkuu wa tarehe 17 - 19 Desemba 2019.
5. Kupokea kutoka kwa Baraza Kuu taarifa ya kazi za Chama kwa kipindi cha miaka mitano
6. Uchaguzi wa viongozi wa kitaifa watakao kiongoza Chama kwa kipindi cha miaka mitano (2021 – 2026). Nafasi zitakazo chaguliwa ni kama ifuatavyo:
   i. Mwenyekiti wa Chama wa Taifa
   ii. Makamu Mwenyekiti wa Chama
   iii. Katibu Mkuu wa Chama
   iv. Mwenyekiti, Katibu, Mweka Hazina na Wajumbe wa Kamati ya Ushauri Wafanyakazi Wanawake Taifa
   v. Wajumbe wa Mkutano Mkuu wa Shirikisho toka TALGWU nafasi 38
7. Mengineyo
8. Kufunga Mkutano.

**NB:**
***Tarehe 26/08/2021 utafanyika uchaguzi wa Viongozi wanaochaguliwa na Baraza Kuu Taifa. Nafasi zitakazo chaguliwa ni kama ifuatavyo:***

i. Mweka Hazina wa Chama
ii. Wadhamini wa Chama nafasi nne (4)
iii. Wajumbe wa Baraza Kuu wa Shirikisho toka TALGWU nafasi 16
iv. Mjumbe mmoja (1) wa Kamati ya Utendaji ya Shirikisho toka TALGWU
v. Mjumbe mmoja (1) mwakilishi wa watu wenye ulemavu atakaechaguliwa miongoni mwa wawakilishi wa Mikoa kuingia Kamati ya Utendaji ya Taifa.
vi. Mjumbe mmoja (1) mwakilishi wa Wafanyakazi Vijana atakaechaguliwa miongoni mwa wawakilishi wa Mikoa kuingia Kamati ya Utendaji ya Taifa.

**Imetolewa na**

**Rashid M. Mtima**
**Katibu mkuu – TALGWU**
**Tangazo hili linapatikana pia katika website ya Chama: www.talgwu.or.tz**

116403501



**The Guardian Limited**

**VACANCY**

**Freelance Sales Executives**

**The Guardian Limited** is looking for self driven sales personnel to join our **advertising** Sales Team in **Dar es Salaam, Dodoma, Arusha, Zanzibar, Tanga, Morogoro and Kilimanjaro.**

**Responsibilities**

- Be responsible for aggressive development of new clients and growing existing business.
- Proactively develop new business avenues
- Devise and monitor business plans to ensure substantive sales
- Develop strategic solutions that meet the unique needs of each client

**Qualifications**

- The position requires someone who can deliver the set targets within deadlines under competitive working environment.
- Applicants need to be highly organized, self-motivated with a positive attitude, and can thrive on setting and reaching new goals.
- Holders of a University degree or Diploma in Business Administration
- Experience in Sales and Marketing is an added advantage

**NOTE: This is a commission Based Position**

**Please send your application via Email to vacancy@guardian.co.tz before 15th August, 2021.**

61638702

# Naibu Waziri asikitishwa wamiliki ardhi kutolipa gharama za upimaji

**Na Munir Shemweta,** TABORA

NAIBU Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Dk. Angeline Mabula, amesikitishwa na wamiliki wa ardhi mkoa wa Tabora waliopimiwa maeneo yao wakati wa urasmishaji makazi kushindwa kulipia gharama za upimaji kwa wakati, hivyo kushindwa kumilikishwa maeneo.

Akizungumza na watendaji wa sekta pamoja na halmashauri za mkoa wa Tabora jana katika ukumbi wa Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Mwana Kiyungi, Dk. Mabula, alisema haileti maana serikali inaamua kurasimisha makazi lakini wananchi hawaonyeshi mwamko.

Dk. Mabula alisema jambo hilo linakwamisha mipango ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi katika kumilikisha ardhi wananchi.

Alisema lengo la kuanzishwa urasimishaji wa makazi holela ni kutaka kuwamilikisha wananchi makazi yao sambamba na kuwawezesha kiuchumi.

"Hatutaki kuwa na wananchi ambao wamepimiwa maeneo yao halafu kwa makusudi hawataki kulipia gharama za upimaji. Kwa bahati nzuri kamishna hapa Tabora amejitahidi kutoa elimu kwa wananchi," alisema Dk. Mabula.

Hata hivyo, Dk. Mabula aliwataka watendaji wa sekta ya ardhi katika halmashauri na manispaa za mkoa wa Tabora kuhakikisha wanarudi katika maeneo wanayoishi wananchi kutoa elimu kuhusu faida na hasara za kumilikishwa ardhi.

Kamishna wa Ardhi Msaidizi Mkoa wa Tabora, Jabir Singano, alimweleza Naibu Waziri kuwa mkoa wa Tabora umefanya jitihada kubwa ili kukwamua kazi za urasimishaji makazi holela.

Alisema tangu kuanzishwa ofisi yake, viwanja vilivyopimwa ni 12,875 na ankara ambazo wamiliki wake wamelipia ni 935 kati ya ankara 3,747 zilizotolewa.

"Changamoto kubwa katika urasimishaji makazi hapa Tabora ni mwitikio mdogo wa wananchi katika kuchangia gharama za upimaji licha ya baadhi ya kampuni za upimaji kupima viwanja," alisema Singano.

Ofisa Kodi wa Wizara, Rehema Kilonzi, aliwataka watendaji wa sekta ya ardhi mkoa wa Tabora kuhakikisha wanajiwekea mikakati ya ukusanyaji maduhuli ya serikali kupitia kodi ya ardhi pamoja na uingizaji viwanja katika mfumo badala ya kusubiri maelekezo kutoka makao makuu ya wizara.

"Kila mkoa una mazingira yake, hivyo mhamasishe wananchi katika maeneo yenu kulingana na misimu ya upatikanaji fedha, hiyo itarahisisha upatikanaji pesa ya kodi ya ardhi," alisema.

Naye Ofisa Tawala wa Wizara ya Ardhi, Baraka Mraha, aliwahimiza watumishi wa sekta ya ardhi Mkoa wa Tabora kuzingatia sheria, taratibu na kanuni wakati wa utekelezaji majukumu yao na kuwaeleza kuwa wizara haitasita kuchukua hatua kwa wale watakaokiuka taratibu.

Aidha, Mraha alihimiza watumishi wa sekta ya ardhi katika mkoa wa Tabora kujaza OPPRAS kwa wakati na kwa mujibu wa sheria ili kuthibitisha utendaji wao wa kazi.

Naibu Waziri Mabula alikuwa mkoani Tabora kwa ziara ya siku moja kukagua utendaji kazi wa sekta ya ardhi mkoani humo.



Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Dk. Angeline Mabula (wa pili kushoto), akimkabidhi hati ya ardhi, Fatuma Ali Mohamed wakati wa kikao chake na watendaji wa sekta ya ardhi na viongozi wa halmashauri za mkoa wa Tabora jana, akiwa katika ziara ya kukagua utendaji kazi wa sekta hiyo. Kushoto ni Mkuu wa Wilaya ya Igunga, Sauda Mtondolo. **PICHA: MUNIR SHEMWETA**

# Kortini tuhuma za kukutwa na nyara za serikali

**Na Hadija Kitwana**

WAKAZI wawili wa Mburahati, Dar es Salaam, wamefikishwa katika Mahakama ya Hakimu Kisutu wakikabiliwa na shtaka la uhujumu uchumi.

Washtakiwa hao, Vicent Mteleleka (75) mkulima na Christopher Kipilili (51) mfanyabiashara, walifikishwa jana mahakamani hapo kwa tuhuma za kupatikana na nyara za serikali.

Wakili wa Serikali, Sylvia Mitanto, alisoma shtaka linalowakabili watuhumiwa hao mbele ya Hakimu Mkazi Mwandamizi Evodia Kyaruzi.

Katika shtaka hilo, alidai kuwa Agosti 9, mwaka huu, maeneo ya Mburahati Kisiwani, Wilaya ya Kinondoni, Dar Es Salaam, walikutwa na ngozi ya chui yenye thamani ya Sh. 8,050,000 bila kibali ikiwa mali ya serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mitanto alidai kuwa upelelezi wa shauri hilo haujamilika na kuomba tarehe kwa ajili ya kutajwa.

Hakimu Kyaruzi alitoa masharti ya dhamana kuwa kila mshtakiwa awe na wadhamini wawili wanaotambulika na watie saini dhamana ya Sh. milioni 4.5 kila mmoja au kuwasilisha hati ya mali isiyohamishika.

Washtakiwa wameshindwa kutimiza masharti ya dhamana na wamepelekwa rumande. Hakimu Kyaruzi alipanga kesi kutajwa Agosti 24, mwaka huu.

# Vyombo vya habari vyatakiwa kuwa na sera kupinga unyanyasaji kijinsia

**Na Elizabeth Zaya**

NAIBU Waziri wa Habari, Sanaa, Utamaduni na Michezo, Pauline Gekul, amevishauri vyombo vya habari nchini kutengeneza na kuweka sera za kupambana na vitendo vya unyanyasaji wa kijinsia kwenye maeneo ya kazi ya vyombo hivyo.

Alitoa ushauri huo wakati akifunga mkutano wa siku moja uliowakutanisha wadau mbalimbali wa habari uliolenga kujadili namna ya kuwa na sera za kupambana na unyanyasaji wa kijinsia, ulioandaliwa na Internews kwa kushirikiana na Jukwaa la Wahariri Tanzania (TEF).

Alisema endapo vyombo hivyo vitajiwekea sera na kuzitekeleza kwa nguvu itasaidia kwa kiwango kikubwa kupambana na vitendo hivyo na pia itachangia kuongeza ari kwa wanawake ambao ni waathirika wakubwa kufanya kazi kwa bidii na kuchangia uzalishaji katika maeneo yao ya kazi. Pia, Gekul alisema wazazi wana wajibu mkubwa wa kuhakikisha wanawaelimisha watoto wao namna ya kupambana na vitendo hivyo vya unyanyasaji bila uoga na kuvishinda.

"Na sisi wazazi tuna wajibu mkubwa wa kuhakikisha tunazungumza na watoto namna ya kupambana na vitendo hivi vya ukatili wa kijinsia ili wanapokutana navyo wasiogope, kwa kufanya hivi tutashinda," alisema Gekul.

Aliwataka wazazi kuwekeza kwenye elimu ya watoto wao ili wafaulu vizuri katika taaluma zao na kuwa na sifa zinazojitosheleza kwenye taaluma zao ili wanapokuwa wanatafuta ajira wapunguze uwezekano mkubwa wa kuingia kwenye mtego wa vitendo hivyo vya unyanyasaji.

"Wanapokuwa wamefaulu vizuri kwenye taluma zao hii nayo inawasaidia na kuwaepusha kwa kiwango kikubwa kuingia kwenye mitego ya unyanyasaji hasa wanapotafuta ajira na pia itawaweka katika nafasi ya kuheshimika," alisema Gekul.

Alisema endapo mtoto kwenye taaluma yake anapata sifa na vigezo vyote vinavyokidhi kwenye taaluma yake, ni vigumu kupata matatizo hayo ya unyanyasaji wa kijinsia.

"Baadhi ya watoto wanaokumbana na vitendo hivi vya unyanyasaji wa kijinsia hasa makazini baadhi yao huwa hawakufanya vizuri kwenye taaluma zao zilizowaingiza kazini, kwa hiyo inawabidi wawapigie magoti waajiri wao," alisema Gekul.

Mwenyekiti wa TEF, Deodatus Balile, alisema changamoto ya unyanyasaji kwenye baadhi ya vyombo vya habari bado ni kubwa na kwamba inahitaji ushirikiano wa pamoja kupambana navyo.

Kwa upande wake, Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Utangazaji Tanzania (TBC), Dk. Ayoub Rioba, alisema kuna haja kwa vyombo vya habari kuwekeza kwa waandishi wa habari wanawake ili kuwajengea uwezo zaidi wa ushindani kazini.

Dk. Rioba pia alivishauri vyombo hivyo vya habari kuwa na sera zenye uwazi ambazo zitatoa fursa kwa wanaokumbwa na matukio hayo ya unyanyasaji kuyaripoti.

"Bahati mbaya kwenye baadhi ya vyumba vyetu vya habari hawachukulii matatizo kama haya kwa uzito na hivyo kuchangia watu kuogopa kusema wanapokutana na vitendo hivyo," alisema Dk. Rioba.

HABARI KITAIFA

# Watu 126 wapatiwa chanjo corona wilayani Njombe

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

HALMASHAURI ya Wilaya ya Ludewa mkoani Njombe, imetoa chanjo ya Uviko-19 kwa makundi maalumu takribani watu 126 kuanzia Agosti 5 hadi 10.

Akizungumza na Nipashe, Mganga Mkuu wa Halmashauri ya Wilaya ya Ludewa, Dk. Stanley Mlay, alisema ili kuongeza kasi ya uchanjaji, wameamua kuongeza vituo vyingine vinne kutoka vitatu vilivyokuwapo awali.

"Mwitikio ni wa wastani, tangu tumeanza leo ni siku ya nne, serikali ilipendekeza vituo vitatu ambavyo ni Hospitali ya Milo, Lugarawa pamoja na hapa Hospitali ya Wilaya, lakini sisi tumeongeza katika vituo vya afya vyote vinne kwa maana ya Manda, Mlangali na Lubonde," alisema na kuongeza:

"Hii itasaidia kusogeza karibu huduma kwa watu na tunaendelea na uhamasishaji kwa kutumia magari ya matangazo."

Mganga mkuu huyo alitoa wito kwa walengwa wa chanjo hiyo kijitokeza kwa wingi ili kuchanjwa kwa sababu ni salama.

"Huduma inayotolewa ya chanjo ni salama, kwa sababu serikali ipo inazisimamia, kwa hiyo kimsingi wajitokeze ili kupatiwa hiyo huduma pamoja na kwamba ni ya hiari, lakini ni muhimu sana kwa ajili ya kupunguza matatizo ambayo yanaweza yakatokea," alisema Dk. Mlay.

Aliongeza kuwa wameshaona viongozi mbalimbali wakishiriki kuchanjwa chanjo hii na hakuna tatizo lolote, kwa hiyo wajitokeze wapate huduma waachane na taarifa za uzushi ambazo hazijathibitishwa. Dk. Mlay alisema kwamba sayansi imethibitisha kwamba hii chanjo salama, hivyo watu wajitokeze kuchanja.

Wilaya ya Ludewa imepokea dozi zaidi ya 4,700 za chanjo ya Uviko-19 aina ya Johnson Johnson, huku makundi matatu yaliyopendekezwa na Wizara ya Afya wakitokeza, wakiwamo wenye umri wa kuanzia miaka 50 na kuendelea.

# Songwe kutengeneza oksijeni kukabili corona

**Na Thobias Mwanakatwe**

MKOA wa Songwe umetangaza mikakati ya kupambana na ugonjwa wa COVID-19 kwa kuanza kujenga mtambo wa kuzalisha hewa dawa (oksijeni).

Mtambo huo unajengwa katika hospitali ya mkoa huo kwa lengo la kukabiliana na upungufu wa oksijeni endapo mkoa huo utakabiliwa na ongezeko kubwa la wagonjwa wa corona.

Mkuu wa Mkoa huo, Omary Mgumba, alitangaza mkakati huo juzi wakati akitoa maelekezo juu ya umuhimu wa kuongeza jitihada zaidi za kupambana na UVIKO-19, alipokutana na Kamati ya Ulinzi na Usalama Mkoa, viongozi wa kamati ya amani ya mkoa, mila na wanahabari.

Mgumba alitangaza kupiga marufuku mikusanyiko mikubwa ya kijamii, kisiasa na kidini na kusema hairuhusiwi kufanyika kuanzia sasa bila kupata kibali kutoka kwa mkuu wa wilaya ya sehemu husika.

Kuhusu maeneo ya minadani, masoko, maduka alisema yanatakiwa kuhakikisha hatua zote za kujikinga na UVIKO-19 zipo.

Mkuu huyo wa mkoa aliwataka viongozi wa dini katika nyumba zote za ibada kuzingatia njia zote za kujikinga na UVIKO 19 ikiwa ni pamoja na kuwaelimisha waumini wao kwenda kupata chanjo.

Aliwataka Wakurugenzi Watendaji wa Halmashauri kuhakikisha wanatekeleza agizo la kisera la Wizara ya Afya kuhakikisha kila zahanati katika kijiji kuwa na mitungi miwili ya gesi na kwa vituo vya afya na Hospitali za Wilaya na mkoa kuwa na mitungi 15.

Mgumba alimwagiza Kamanda wa Polisi Mkoa wa Songwe, Janeth Magomi, kuhakikisha wasafirishaji wote wa magari wanabeba abiria kwa idadi ya viti vilivyopo kwenye vyombo vyao.

Aidha, aligiza Jeshi la Polisi kuhakikisha wanafuatilia wamiliki wa baa kuwasimamia wahudumu wao kuvaa barakoa na kufuata kanuni zote za mapambano dhidi ya ugonjwa wa Uviko-19.



Naibu Kamishna Mkuu wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), Msafiri Mbibo (wapili kulia), akitoa maagizo mbalimbali kwa viongozi wa mamlaka hiyo ofisi ya TRA eneo la Kyaka, mkoani Kagera juzi, alipofanya ziara ya kikazi mkoani humo, kwa ajili ya kusikiliza changamoto mbalimbali katika mpaka wa Tanzania na Uganda. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Jaji Mkuu aeleza umuhimu kuwapo mahakama za wilaya

**Na Friday Simbaya,** IRINGA

JAJI Mkuu wa Tanzania, Prof. Ibrahimu Hamis Juma, amesema serikali ina mpango wa kujenga mahakama za wilaya katika wilaya 25, ili kusogeza huduma za Mahakama jirani na wananchi pamoja na kupunguza msongamano wa mahabusu katika mahabusu.

Alibainisha hayo wakati wa mkutano kati ya Tume ya Utumishi wa Mahakama na wajumbe wa kamati za maadili za mkoa wa Iringa na wilaya zake.

Alisema kuwapo kwa mahakama hizo kutapunguza muda wa mahabusu kukaa mahabusu, na kuongeza kuwa mahakama hizo zikiwa mbali na magereza, magereza zitalazimika kusafirisha mahabusi na wakati mwingine kushindwa kuwafikisha mahakamani, kutokana na ukosefu wa fedha.

Prof. Juma alizitaka wilaya zote ambako zinajengwa mahakama za wilaya kuhakikisha wanajenga pia magereza ya wilaya ili kusongeza huduma za mahakama karibu na wananchi, ili baadaye kupunguza msongamano wa mahabusu ambao unasababisha kuchelewa kwa kesi.

Alisema mahakama nchini zinafanya kazi kuanzia Jumatatu hadi Ijumaa na pengine katika wilaya hufanya kazi kwa siku tatu kwa wiki kwa kuwa mahabusu wanashindwa kupelekwa mahakamani.

Aliongeza kuwa msongamano wakati mwingine katika mahabusu husababishwa na kutokuwapo kwa mahakama za wilaya ambapo mahakimu hulazimka kufanya kazi mara tatu kwa wiki, kutokana na kutokuwapo na magereza karibu na mahakama.

Wakati huo huo, Prof. Juma amewaagiza Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Prof. Adelaradus Kilangi, kutafuta andiko la mwaka 2010 ambalo liliziagiza wilaya zote nchini kujenga magereza.

Alisema ni vizuri mwanasheria huyo wa serikali akalifufue andiko hilo la kujenga magereza ili mahakama iweze kutoa haki kwa wakati kwa kuwa mahabusi watafikishwa mahakamani kwa haraka.

Jaji mkuu anafanya ziara ya kutembelea kamati za maadili katika mikoa ya Iringa, Njombe, Mbeya na Songwe pamoja na kutembelea miradi mbalimbali ya kujenga miundombinu ya Tehama, ili mahakama ziweze kuendesha mashauri kwa mfumo wa mtandao katika kipindi hiki cha COVID-19.

# Sakata uchomaji mikorosho ya diwani sasa laibuka upya

**Na Hamisi Nasri,** MASASI

TUKIO la kukatiwa mikorosho zaidi ya 50 ya diwani mstaafu wa Namwanga Halmashauri ya Wilaya ya Masasi mkoani Mtwara, Edwin Kasembe, limetinga kikao cha Baraza la Madiwani na kuzua mvutano mkubwa.

Madiwani wamemtaka diwani wa sasa wa kata hiyo kujieleza kwa nini tukio hilo halijaingizwa katika taarifa yake.

Wakiwa katika kikao cha Baraza la Madiwani robo ya nne kilichofanyika jana mjini Masasi, madiwani walikuja juu na kumtaka diwani wa sasa, Yusuph Mlaponi, kujieleza kwa nini wakati wa uwasilishaji wa taarifa ya maendeleo ya kata yake haijawekwa taarifa ya kukatwa kwa mikorosho zaidi ya 50 ya diwani mstaafu.

Diwani wa Chikoropola, Edward Mehelela, alisema sakata hili linaibuliwa sasa kutokana na chuki za kisiasa.

Alisema imebainika kuwa hakuna maelewano mazuri kati ya kundi la diwani wa sasa na kundi la diwani aliyemaliza muda wake, hivyo hali hiyo inapelekea hata tukio la ukataji wa mikorosho hiyo kuhusishwa na mambo ya kisiasa kati yao.

Mahelela alisema kitendo cha taarifa ya maendeleo ya Kata ya Namwanga ya kipindi cha miezi mitatu iliyopita kuwasilishwa na kusomwa mbele ya madiwani bila ya kugusia ukataji wa mikorosho ya diwani mstaafu ni jambo ambalo sio sahihi na ni dharau kwa madiwani.

Naye Diwani wa Mijelejele, Juma Pole, alisema wanataka kufahamu sababu iliyopelekea kutowekwa taarifa ya ukataji mikorosho kwenye taarifa ya maendeleo ya Namwanga wakati tukio hilo lilitokea kwenye kata hiyo.

Pole alisema wanafahamu na walitarajia kuwekwa kwenye taarifa ili waweze kuijadili kwa mapana, hivyo wanashangazwa na majibu yanayotolewa na diwani husika kuwa haijawekwa kwa sababu mhusika tangu mikorosho yake ikatwe hajalifikisha tukio ofisi ya kijiji na kata.

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Masasi, Ibrahimu Chiputula, alisema kitendo cha diwani wa Namwanga kutoa majibu ambayo sio sahihi kwa madiwani kuhusu hoja ya kutaka kufahamu suala la ukataji wa mikorosho na anapaswa kueleza wazi kilichotokea.




Mkuu wa Kitengo cha Biashara Benki ya ACB, Webster Kaunga (kulia), akishirikiana na Mkuu wa Idara ya Mikopo, Charles Kamoto, kuzindua huduma ya wakala wa benki hiyo, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wafanyabiashara waonywa kuchezea vipimo

**Na Mwandishi Wetu,** GEITA

WAKALA wa Vipimo (WMA), imewaonya wafanyabiashara kujiepusha na vitendo vya kuchezea vipimo, kwani kufanya hivyo wanaweza kutozwa faini hadi Sh. milioni 100.

Hayo yalisemwa jana mkoani Geita na Meneja wa WMA mkoani hapa, Moses Ntungi, kwenye maonyesho ya kuhamasisha utalii na biashara wilayani Chato.

Alisema kuchezea vipimo ni kosa na ni kinyume na Sheria ya Vipimo Sura na. 340 na mapitio yake ya mwaka 2002 na kwamba endapo mfanyabiashara atakamatwa kwa udanganyifu wa vipimo na kukiri makosa yake atapigwa faini isiyopungua Sh. 100,000 na isiyozidi Sh. milioni 20.

Alisema endapo mtuhumiwa atakataa na kufikishwa mahakamani kama mkosaji wa kosa la kwanza atatozwa faini isiyopungua Sh. 300,000 na isiyozidi milioni 50 au kifungo kisichozidi miaka miwili au vyote kwa pamoja.

Ntaungi alisema pia endapo mtuhumiwa atakuwa na makosa ya kujirudia atatozwa faini isiyopungua Sh. 500,000 na isiyozidi Sh. milioni 100 au kifungo kisichozidi miaka mitano au vyote kwa pamoja.

Alisema lengo kuu la WMA kushiriki katika maonyesho hayo ni kutoa elimu kwa umma kuhusu matumizi sahihi ya vipimo kwenye sekta mbalimbali.

Alisema uwepo wa maonyesho hayo kumesaidia wananchi wa Wilaya ya Chato kujifunza mambo mbalimbali na kazi zinazofanywa na Taasisi ya WMA ikiwa ni pamoja na kutambua umuhimu wa kutumia vipimo sahihi pamoja na kutambua vipimo vilivyohakikiwa na vile visivyohakikiwa (batili).

Ntungi alieleza kuwa vipimo vyote vilivyohakikiwa na WMA huwekewa alama maalumu ambayo ni stika inayosaidia mtumiaji wa kipimo kutambua kwa urahisi kama kipimo anachotumia kipo sahihi na kimehakikiwa.

## CHAVITA yaomba elimu chanjo corona

**Na Christina Haule,** MOROGORO

CHAMA cha Viziwi Tanzania (CHAVITA) mkoa wa Morogoro kimeiomba serikali kuona haja ya kuwapa elimu juu ya chanjo ya ugonjwa wa corona kabla hawajachanja.

Lengo ni kuwaondolea woga kuhusiana na chanjo hiyo.

Katibu wa CHAVITA Mkoa wa Morogoro, Salumu Ally, alisema hayo jana wakati akizungumza na waandishi wa habari, na kueleza kuwa hawajapata elimu ya chanjo ya UVICO- 19, na kwamba kama watapewa elimu hiyo kwa pamoja, itawasaidia kutambua umuhimu wake na kujitokeza kuipokea.

Ally alisema wakikusanywa pamoja, watu wenye ulemavu wa kutosikia 427 waliopo mkoa mzima wa Morogoro wakiwamo watu wazima 350 na kupewa elimu juu ya chanjo hiyo wataelimika na ndipo wengine wataenda kuwa mabalozi kwenye wilaya zao kwa kuelimisha wenzao na kuitikia wito wa kuchanja mahali walipo.

## Wazazi CCM kujenga jengo kitega uchumi

**Na Julieth Mkireri,** KIBAHA

JUMUIYA ya Wazazi wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), inatarajia kuanza ujenzi wa nyumba ya katibu wake pamoja na kitega uchumi kwa gharama ya Sh. milioni 55.

Akizungumza na Nipashe mjini Kibaha, Mwenyekiti wa Jumuiya hiyo, Nuru Magege, alisema ujenzi wa majengo hayo unatarajia kuanza mwezi huu.

Nuru alisema kukamilika kwa kitega uchumi hicho kitaisaidia jumuiya kuondokana na utegemezi kutoka kwa wadau ambao wamekuwa wakiwafadhili kwa kila jambo wanalopanga kufanya.

Aidha, alisema kabla ya kukamilika kwa kitega uchumi hicho wanatarajia kuanza mradi wa kukodisha maturubai na viti ambao utaanza hivi karibuni.

Mwenyekiti huyo aliomba wadau wa ndani na nje ya Wilaya ya Kibaha kujitokeza kufanikisha mipango hiyo kwa michango ya fedha na vifaa.

**SAIF AL-ISLAM GADDAFI**
Licha ya kuzushiwa kufa, yu hai akitamani urais



Ukurasa 14



Ukurasa 12

**MWINYI Vs UONEVU ZANZIBAR**



Ukurasa 12

**TEHAMA inavyosaidia kupunguza gharama za ununuzi serikalini**

siasa
JUMATANO AGOSTI 11, 2021
Nipashe
HABARI BORA NA KAMILIFU

# KUKATAA CHANJO CORONA

## • Polepole anapoonekana mpinzani

**Na Sabato Kasika**

WACHAMBUZI wa masuala ya kisiasa wanamtizama katibu wa zamani wa Itikadi na Uenezi wa CCM taifa, Humphry Polepole, kuhusu kile alichoandika kwenye mitandao ya kijamii kuikataa chanjo ya COVID-19. Wanaona kuwa anaweza kuwachanganya wananchi kwa vile ana wafuasi wengi ndani ya jamii. Lakini pia anachosema kinapinga maelekezo ya bosi wake na Mwenyekiti wa CCM.

Wakitoa maoni kufuatia andiko lake ambalo amelipa kichwa cha habari, Kalamu ya Humphrey Polepole, amezungumza mengi, akitaja msimamo wake kuwa kuishinda hofu ni silaha muhimu zaidi dhidi ya virusi vya corona.

Lakini, pia anaandika kuwa ni nyenzo muhimu ya kuimarisha uchumi na kuleta maendeleo kwa watu, huku akiipongeza serikali kuweka uchumi sawa katika kipindi hiki kinachoitwa wimbi jingine la corona mwaka 2021.

Aidha, anataka mbinu moja isiachwe, kwamba corona si kubwa kama ambavyo Watanzania wanaambiwa akiendelea kusema: 'Mungu ibariki Tanzania, ibilisi na huu ugonjwa wake hawana nafasi Tanzania'.

Pamoja na hayo, kilichowaibua wadau na wachambuzi wa siasa kwenye maoni ya polepole ni hiki; 'kuchanja ni hiari, lakini siyo kila kitu, mimi nitaimarisha kinga ya mwili wangu na chanjo kwangu HAPANA. Sasa baadhi yenu msihangaike na mimi, hangaikeni na rai yangu hapo juu'.

Kutokana na hicho alichoandika mwanasiasa huyo ambaye pia ni mbunge wa kuteuliwa, baadhi ya wanasiasa na wachambuzi wanazungumza na Nipashe na kutoa maoni yao yao jinsi wanavyochukulia andiko hilo.

### MAZINGIRA YA SINTOFAHAMU

Mchambuzi wa siasa, Said Msonga, anasema, alichoandika mwanasiasa huyo kwenye mitandao ya kijamii, ni sawa na kupingana na maelekezo ya serikali yanayotolewa na Rais na Mwenyekiti wa CCM Taifa, Rais Samia Suluhu Hassan.

"Ninasema anapingana na msimamo, kwa sababu tayari msimamo ulishatolewa kuwa chanjo ni hiari, sasa yeye alikuwa na sababu gani kuandika tena jambo hilo hilo? Inaweza kusababisha mpasuko," anasema Msonga.

Msonga anaona kuwa kilichoandikwa na Polepole ni tatizo tena ni kwenda kinyume na uwajibikaji wa pamoja, na kwamba kauli hiyo inaonyesha kuwa huenda kuna ajenda nyingine zaidi ambayo iko nyuma ya pazia.

"Polepole ni kiongozi ambaye kama anapingana na msimamo wa viongozi wenzake, angekwenda katika vikao husika badala ya kujitokeza hadharani na kuandika vitu ambavyo vinaashiria kupingana na serikali na chama ambavyo yeye ni sehemu ya jumuiya hiyo," anasema.

Anakumbusha kuwa Polepole alishakuwa kiongozi wa juu wa CCM na sasa ni mbunge wa kuteuliwa, na kwamba anajua taratibu zote za kiuongozi, ila anamshangaa kwa nini ameshindwa kuzitumia kufikisha ujumbe wake.

"Miongoni mwa taratibu hizo ni kutumia vikao halali kupeleka jambo ambalo anaona kuna haja ya kulijadili, ili hata kama maamuzi yatakosewa au kuwa sahihi yawe ya wote, kwa kuwa huo ndiyo uwajibikaji wa pamoja," anasema.

### HAJAKOSEA, YUKO SAHIHI

Gwandumi Mwakatobe, ni mchambuzi mwingine wa siasa, ambaye anasema, mwanasiasa huyo hajafanya kosa kutoa maoni yake kwenye mitandao ya kijamii, kwa kuwa katiba ya nchi inaruhusu uhuru wa kutoa maoni.

"Ametumia uhuru wake wa kutoa maoni vizuri ambao umo katika ibara ya 18 ya katiba ya nchi yetu iwe ni kukubali au kupingana na serikali, kwani yeye ni mbunge tu siyo waziri," anakumbusha Mwakatobe.

Mchambuzi huyo wa siasa anasema, Polepole hajasema kinyume na kile ambacho serikali imeelekeza kuhusu chanjo kuwa ni hiari, na kwamba yeye ametumia uhuru kutoa msimamo wake kwa kueleza kuwa hatakwenda kuchanjwa.

" Watanzania hatuna utamaduni wa kukosoa serikali, ndiyo maana baadhi ya watu wanaamini kwamba amefanya kosa, lakini ametumia uhuru ambao umo ndani ya katiba kutoa maoni yake," anasema na kukumbusha kuwa kila mmoja ana haki ya maoni.

Anafafanua kuwa kinachoendelea sasa, ni mabishano kati ya wanaochanjwa na wasiochanjwa, na kwamba kila kundi linajiona liko sahihi halitaki kukosolewa bila kuangalia ni wapi viongozi wetu walikosea.

"Nikumbushe tu kwamba, Polepole hajatoka nje ya tamko la serikali, yuko sahihi kabisa, ila pia ni vyema kutowaona wasiochanjwa au wanaochanjwa kuwa wamekosea, kwa kuzingatia kwamba chanjo ni hiari," anasema.

### KWANINI ASHAMBULIWE?

Naibu Katibu Mkuu wa CUF Bara, Magdalena Sakaya, anasema anasikitishwa Umoja wa Vijana CCM (UVCCM) kumwandama mwanasiasa huyo baada ya kutoa maoni yake ambayo hayaendani na msimamo wa serikali ambayo yeye ni sehemu ya muhimili wa dola unaounda serikali hiyo ambao ni bunge.


"Katibu Mkuu wa UVCCM Kenani Kihongosi, anasema wanasikitishwa na matendo yanayofanywa na mbunge Humprey Polepole kuhusu suala la chanjo, " kwani amekosea wapi? Ni kama wanamuonea tu," anasema Sakaya.



Pole Pole akizungumza kwenye moja ya mikutano ya kikazi. **PICHA: MTANDAO**

INAENDELEA UK.14

# TEHAMA inavyosaidia kupunguza gharama za ununuzi serikalini



Maboresho katika Bandari ya Dar es Salaam kumeusaidia GPSA kuongeza kuongeza ufanisi na tija katika utoaji wa huduma na utendaji kazi. **PICHA: MTANDAO**

**Na Mwandishi Wetu**

MOJAWAPO ya mambo ambayo wabunge na wasimamizi wengine wa fedha za umma wanayalalamikia ni gharama na upotevu wa fedha za serikali , hasa wanapochambua ripoti za Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG).

Wadau hao wanataka jitihada mbalimbali zichukiuliwe ikiwamo kutumia teknolojia kupunguza au kukomesha tatizo hilo.

Jitihada za kupunguza gharama na upotevu kwenye ununuzi wa umma zinafanywa kupitia Wakala wa Huduma ya Ununuzi Serikalini (GPSA), ambao unajikitika katika mifumo ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA), ili kuongeza ufanisi na tija katika utoaji wa huduma na utendaji kazi.

Akizungumza na Nipashe, Ofisa Mtendaji Mkuu wa GPSA, Prof. Geraldine Rashel, anasema uwekezaji huo unaboresha huduma ya uondoshaji mizigo ili kuhudumia wateja wenye uhitaji maalum na mkubwa.

Wakala unalenga kununua, kutunza na kusambaza vifaa mtambuka na mafuta ya magari kwa taasisi za serikali na kuondoa shehena za serikali bandarini, viwanja vya ndege na mipakani, anaongeza.

Aidha, itakuwa inatoa uhifadhi salama wa vifaa na mali za taasisi za umma kitaalamu, ununuzi wa pamoja wa magari ya serikali, kutoa ushauri wa kitaalamu katika nyanja za ununuzi, ugavi na uondoaji mizigo na kutoa orodha ya wazabuni wa vifaa na huduma mtambuka (VHM).

"Kwa miaka minne, GPSA imefanyakazi kwa mafanikio ikiwamo kununua, kutunza na kusambaza vifaa mtambuka na mafuta ya magari kwa taasisi za serikali,"anabainisha Profesa Rashel na kuongeza kuwa yamefanyika maboresho ya muda kama kutoa mafuta kwa magari ya serikali ndani kila siku zikiwamo na sikukuu za kitaifa katika vituo vyote.

> Kwa sasa mchakato huu wa kupata wazabuni wa VHM unafanyika kupitia mfumo wa kielektroniki wa ununuzi wa TANePS kupitia anuani ya 'www.taneps.go.tz'.

Anasema wakala umeboresha upatikanaji wa vifaa katika maghala yake kwa kiasi kikubwa katika mikoa yote Bara ikiwamo vifaa vya shule za msingi na sekondari kwa bei ya ushindani, ili kuipunguzia serikali gharama.

Kadhalika, wakala unatekeleza kazi zake kwa mujibu wa kifungu cha 50, kanuni ya 131 (4)(a), ya utaratibu wa kuwa kituo maalum 'One Stop Centre' kwa ajili ya ununuzi wa magari ya serikali, kutoa taarifa zote zinazohusu magari, watengenezaji na wazabuni, hivyo kuongeza uwazi na uwajibikaji katika eneo hilo.

### KUOKOA MAPATO

Anasema kwa miaka minne, inakadiriwa kuwa serikali imeokoa zaidi ya Sh. milioni 18.5 baada ya kuepuka gharama za michakato ya ununuzi ikiwa kila taasisi ingekuwa inafanya ununuzi wenyewe.

Profesa Rashel anabainisha kwamba GPSA, inatekeleza jukumu hilo kwa mujibu wa Waraka wa Hazina namba 3 wa mwaka 2014/15, kifungu 50, kanuni ya 131.

"Utaratibu huu umesaidia kuokoa gharama za michakato ya zabuni kwa taasisi za umma kila zinapohitaji vifaa mtambuka, pia hii ni fursa ambayo wakala imetoa kwa wazabuni na taasisi binafsi kuweza kufanya biashara na Serikali" anasema Rashel .

Kwa utaratibu huo, katika miaka minne, serikali inakadiriwa kuokoa zaidi ya Sh. bilioni 308.966 na idadi ya wazabuni waliokidhi vigezo na kupewa mikataba maalum kwa ajili ya kufanya kazi na taasisi za serikali inakadiriwa kuwa 44,777, anaongeza.

Anasema kwa sasa mchakato huu wa kupata wazabuni wa VHM unafanyika kupitia mfumo wa kielektroniki wa ununuzi wa TANePS kupitia anuani ya 'www.taneps.go.tz'.

Anabainisha kuwa jukumu hilo linatekelezwa kupitia kanuni ya 130 (5), kwamba wakala umeweza kugomboa mizigo kwa niaba ya taasisi za serikali kwa usalama, uhakika na gharama nafuu kutokana na uzoefu na weledi mkubwa wa watumishi.

Anasema katika miaka minne, GPSA imegomboa mizigo ya serikali inayokadiriwa kuokoa zaidi ya Sh. bilioni 9.6 kutokana na tozo nafuu pamoja na kuokoa gharama za michakato ya ununuzi.

### MIPANGO IJAYO

Akizungumzia mipango ya baadaye ya wakala, Prof. Rashel anasema wakala umejiwekea mipango mbalimbali ili kuendelea kutoa huduma kikamilifu, kuhakikisha unaleta tija hasa katika eneo la ununuzi.

Anayataja maeneo hayo kuwa ni kushirikiana na sekta binafsi na umma katika usambazaji wa vifaa mbalimbali, kuondosha mizigo,wakala kuendelea kuagiza vifaa kutoka kwa wazalishaji wa ndani na nje ya nchi ili kuweza kuvipata kwa nafuu zaidi kutokana na kununua vifaa kwa uwingi.

"Wakala utazidi kusogeza huduma kwa wateja wake mpaka ngazi ya wilaya, kwamba mpaka sasa wakala umefungua ofisi ndogo katika Wilaya ya Ileje mkoani Mbeya, ofisi ndogo wilaya ya Kahama katika Mkoa wa Shinyanga na kuendelea kuongeza wilaya zingine, kwa sasa tuko katika mpango wa kujenga ofisi za wilaya katika mikoa ya Iringa na Tanga," anasema Prof.Rashel.

Ofisa Mtendaji Mkuu huyo anasema wakala pia utaendelea kufanyia maboresho na kujenga miundombinu yake ikiwamo ujenzi wa miundombinu ya kuhifadhia mafuta yatakayonunuliwa moja kwa moja kutoka kwa wazalishaji, lengo likiwa ni kununua mafuta kwa bei rahisi, hivyo kuziuzia taasisi za umma kwa bei ndogo.

Anasema kwa kuzingatia ukuaji mkubwa wa matumizi ya TEHAMA, GPSA itaendelea kuwekeza katika mifumo ya hiyo ili kuongeza ufanisi na tija katika utoaji wa huduma na utendaji wa kazi.

Prof. Rashel anasema: "Wakala umeboresha na kuendelea kuboresha huduma ya ugomboaji na uondoshaji mizigo ambapo mpaka sasa wakala umeongeza vifaa na watumishi ili kuweza kuhudumia wateja wenye mahitaji maalum na makubwa".

GPSA ilianzishwa kwa sheria ya uanzishwaji wakala za Serikali namba 30 ya 1997, kupitia Tangazo la Serikali namba 235, la Desemba 2007 na kuzinduliwa Juni 2008 kuchukua majukumu ya iliyokuwa Bohari Kuu ya Serikali.

# MWINYI Vs UONEVU ZANZIBAR

• Anaonyesha utashi wa kisiasa kupinga udhalilishaji kijinsia

**Na Reubeni Lumbagala,**

**DODOMA**

KWA wanaofuatilia masuala ya haki na ustawi wa watoto na wanawake changamoto kubwa eneo hilo ni udhalilishaji na ukatili wa kijinsia ulioshamiri dhidi yao.

Wakati mwingine inaonekana kuwa ili kuutokomeza na kulinda haki ya kundi hilo ni lazima kuwepo na utashi wa kisiasa, kwa maana kuwa ni lazima mambo yaanze Ikulu ili wahusika wengine wawajibike.

Kushamiri kwa vitendo vya udhalilishaji wa wanawake na watoto, kunaziibua serikali na taasisi za kijamii (NGOs) kuweka mikakati mbalimbali ya kupambana na ukatili huo ikiwamo kuhamasisha watoto na wanawake kutoa taarifa za matukio, kuwafikisha watuhumiwa mahakamani na kuwa na kuwaadhibu.

Visiwani Unguja na Pemba ni miongoni mwa maeneo ambayo vitendo vya ukatili wa wanawake na watoto vimeshamiri, hali inayohatarisha ustawi wa wanawake na watoto na maendeleo kwa ujumla.

Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti Dk. Hussein Ali Mwinyi, amedhihirisha umuhimu wa kuwapo utashi wa kisiasa na hivi karibuni, ametangaza rasmi vita kwa watendaji na viongozi watakaobainika kushiriki vitendo vya udhalilishaji.



Rais Mwinyi ametangaza kuchoshwa na tatizo sugu la unyanyasaji kijinsia. **PICHA: MTANDAO**

Anawaambia kuwa wao wanapaswa kuwa mstari wa mbele katika kuleta matokeo chanya ya mapambano dhidi ya maovu haya na kukumbusha kuwa ustawi wa watu na maendeleo ya nchi unategemea uongozi bora na wanaoheshimu haki za binadamu.

Rais Mwinyi anasema hayo katika hafla ya kuipongeza Taasisi ya The Foundation for Civil Society (FCS) kutokana na mchango wake wa kupinga ukatili wa kijinsia katika kongamano la harakati za kutokomeza vitendo vya udhalilishaji linaloandaliwa na Jumuiya ya Wanawake Wanasheria Zanzibar (ZAFELA).

Rais Mwinyi anasema atamchukulia hatua mtendaji yeyote aliyemteua ambaye atabainika kujihusisha na vitendo vya udhalilishaji na ukatili dhidi ya wananchi ambao anatakiwa kuwahudumia na kuwaongoza

Aidha, Rais Mwinyi anaonyesha kusikitishwa kwake na baadhi ya wateule wake kuwa washirika wa vitendo hivyo bila kuchukuliwa hatua stahiki.

"Ukiyasikia haya yanasemwa hapa mimi binafsi napata huzuni kubwa kwa sababu inaonekana taasisi zinazotakiwa kufanya kazi zao hazitimizi wajibu kikamilifu na zina watuhumiwa wanajulikana lakini wapo wanaendelea kutazamwa bila ya kuchukuliwa hatua."

Watendaji na viongozi wamepewa dhamana kusimamia taratibu, sheria na kanuni za nchi na za mataifa ili dunia iwe mahali bora pakuishi na kuwe na ustawi na maisha bora ya watu ili kufikia malengo ya raia na yale ya kitaifa.

Baadhi ya watendaji na viongozi wanaposhindwa kusimamia wajibu wao wa msingi wa kufanya hivyo, ni dhahiri wanakuwa wamekwama katika kazi walizoaminiwa na mamlaka za uteuzi na kuchaguliwa na wananchi, na hivyo, hawana budi kupisha wengine wenye uwezo wa kusimamia majukumu yao ipasavyo.

Taifa litaendelea kusuasua kwenye kupiga hatua za kimaendeleo katika nyanja za kiuchumi, kiafya, kijamii, kielimu na kisiasa kama kundi hili muhimu la wanawake na watoto litaendelea kufanyiwa ukatili na udhalilishaji.

Ni dhahiri ukatili na udhalilishaji unarudisha nyuma maendeleo yao kwa vile unakuwa ni chanzo cha madhila mengi yakiwamo maradhi ya akili, ulemavu, mimba za utotoni, na kuumizwa miili, maradhi yakiwamo ya ngono na VVU.

Rais Mwinyi, anaona kuwa ukatili huu ni mkwamo kwa wanawake na anawataka watendaji na viongozi wafahamu kuwa wana wajibu wa kushiriki kikamilifu katika mapambano haya ili kutokomeza vitendo vya ukatili na udhalilishaji.

> Mambo ambayo yanapigwa vita ni pamoja na kuwapiga wanawake, ubakaji, ulawiti na ukatili kwa watoto...

Mambo ambayo yanapigwa vita ni pamoja na kuwapiga wanawake, ubakaji, ulawiti na ukatili kwa watoto ambao ni kikwazo katika maendeleo yao na kupatikana maendeleo ya nchi.

Aidha, Rais Mwinyi anaonyesha kusikitishwa kwake na vitendo vya wanaume kuwapiga wake zao na anakemea tabia hiyo na kuwaasa wanaume kuacha mienendo hiyo kwani hata imani za dini zina utaratibu wake katika suala la mwanaume kumpiga mke wake.

Taasisi ya The Foundation for Civil Society (FCS) inatoa mchango mkubwa Zanzibar katika mapambano ya ukatili na udhalilishaji ili kuleta ustawi na maendeleo katika visiwa vya Pemba na Unguja, kwa mujibu wa Mkurugenzi Mtendaji wa FCS Francis Kiwanga.

"Miongoni mwa kazi kubwa iliyofanywa na FCS Zanzibar kwa miaka mitano iliyopita ni pamoja na kutoa ruzuku yenye thamani ya Shilingi bilioni 4.09 kwa mashirika 73 yanayofanya kazi katika sekta za maboresho ya sera, haki za ardhi kwa wanawake, kupinga ukatili wa watoto, ushiriki na ushirikishwaji wa jamii katika maendeleo.

"Mengine ni ajira kwa vijana, ujenzi wa amana na utatuzi wa migogoro, kuchangia katika mchakato wa uaandaji wa rasimu ya sheria ya NGO na ukusanywaji wa maoni ya wadau na jumuiya kutoka Pemba na Unguja."

Anasema pamoja na kwamba watendaji na viongozi wana jukumu la kusimamia kikamilifu mapambano ya ukatili wa kijinsia na udhalilishaji, bado mchango wa wananchi ni muhimu katika kufikia matokeo chanya ya mapambano haya.

Anasema ukatili na udhalilishaji unafanyika ndani ya familia na jamii, hivyo wahusika hao wanapaswa kuwafichua wale wote wanaofanya vitendo vya ukatili na udhalilishaji kwani kwa kufanya hivyo watuhumiwa watapata funzo na kuachana na tabia hiyo, hatimaye kuyafikia maendeleo ya kweli.

***Reubeni Lumbagala ni Mwalimu wa Shule ya Sekondari Mlali ya wilayani Kongwa, Mkoa wa Dodoma. Maoni: 0620-800462***

# Kukataa chanjo corona

**INATOKA UK.11**

Polepole anasema kama binafsi, kutokana na kwamba kwa sasa hayuko kwenye madaraka makubwa ya kushawishi watu wasichanjwe, bali yeye na familia yake hawatachanjwa, ndilo analosema, anaongeza Sakaya.

"Chanjo ni hiari, ameamua kuwa yeye na familia yake hawachanji, hapo kosa liko wapi, huyo kiongozi wa UVCCM anataka Polepole afanye kipi ili ionekane haendi kinyume na Rais Samia Suluhu Hassan? Anahoji.

Sakaya anamtaka kiongozi huyo wa UVCCM kutowalazimisha watu kwenda kuchanja, kwa kuwa kufanya hivyo ni kwenda kinyume na maelekezo ya serikali ambayo yanaruhusu Watanzania kuchanjwa au kutochanjwa.

**ONYO LA UVCCM**

Polepole amekuwa mbunge wa pili kwa makada wa CCM kutamka hadharani kupinga chanjo akiwa ametanguliwa na mbunge wa Kawe, Askofu Josephat Gwajima, ambaye naye alishaonywa na umoja huo.

Kwa Polepole, katibu huyo anasema, wanasikitishwa na matendo suala la chanjo, kwa kuwa Mwenyekiti wa CCM taifa Rais Samia, ameshasema chanjo ni hiari na umaamuzi wake lazima uyaheshimiwe.

"Tunapenda kumwambia mbunge Polepole kwamba awe na nidhamu na adabu kama aliyokuwa nayo wakati wa utawala wa awamu ya tano, nidhamu ileile aiendeleze pia katika utawala huu wa awamu ya sita inayoongozwa na Rais Samia Suluhu Hassan, mijadala yake kuhusu chanjo ni bora akakaa kimya kama haitaji kuchanja, lakini sio kujificha katika kivuli cha chanjo kuipinga serikali," anasema Kihongosi.

Kuhusu kauli ya Gwajima, katibu huyo aliwahi kuweka wazi kuwa kamwe UVCCM haitavumilia utovu wowote wa nidhamu kwa Rais na serikali yake, kwa watu kuendelea kutengeneza maneno ya kejeli, dhihaka na mengine ya aina hiyo yanayobeba mazingira yanayotia shaka.

Kihongosi akadai kuwa Mbunge huyo ametoa maneno ya kichochezi na kwamba yanakwenda kuwagawa wananchi kwa kuwa Rais ameshatoa msimamo kwa wananchi wapate chanjo.

Akafafanua kuwa utaratibu alioutumia mbunge huyo wa kwenda kutoa maneno hayo kwa umma, kuwa mtu atakayediriki kuwaambia watu wachanjwe atakufa ni utovu wa kinidhamu.

"Sisi Umoja wa Vijana wa Chama Cha Mapinduzi kauli zile tunazipinga na kuzilaani kwa sababu utaratibu wa CCM unafahamika kama mbunge ana jambo lake anapeleka kwenye kamati ya wabunge wa chama," anasema.

JUKWAA LA UONGOZI

# SAIF AL-ISLAM GADDAFI

- Bin Gadaffi anayetaka kuiongoza tena Libya
- Licha ya kuzushiwa kufa, yu hai akitamani urais
- Ni baada ya miaka 10 ya kifo cha baba yake

Na Mwandishi Wetu

MIAKA 10 baada ya kuuawa kiongozi wa Libya Muamar Gaddafi , mtoto wake wa kiume Saif al-Islam, amejitokeza hivi karibuni na kusema anataka ridhaa ya Walibya ili arejea nyumbani na kuwania urais wa taifa lao .

Hatua hiyo ya Islam imezua mjadala nchini mwake iwapo kuna majuto miongoni mwa Walibya kuhusu yaliyomsibu kiongozi wao wa miaka zaidi ya 40 Kanali Gaddafi.

Hadi sasa bado haijulikani athari za hatua ya Islam kutaka kurejea Libya na kuwa kiongo miaka 10 baada ya babake na baadhi ya kakake zake kuuawa katika mapinduzi ya umma.

Saif al-Islam, kutangaza nia ya kutaka "kurejesha umoja" nchini humo baada ya kukaa mafichoni kwa miaka kadhaa, analiambia gazeti la Marekani la New York Times kuwa anataka kugombea uraisi.

Islam, katika mahojiano na gazeti hilo la Marekani, anazungumza kuhusu mambo mengi yanayohusiana na nchi hiyo ya Kaskazini mwa Afrika ya Libya pamoja na siasa na kueleza nia hiyo ya kugombea urais na kuongoza nchi yake.

Itakumbukwa kuwa Agosti 2011, takribani muongo mmoja sasa waasi walidhibiti mji mkuu wa Libya Tripoli wakati huo baba yake Islam, aliendelea kujificha lakini alikamatwa na kuuliwa katika uasi na upinzani dhidi yake ulioongozwa na majeshi ya NATO.

Saif al-Islam, aliyewahi kufikiriwa kuwa mrithi wa baba yake, anasema viongozi wa Libya "hawajaleta chochote ila mateso" kwa watu nchini humo tangu wachukue nchi miaka 10 iliyopita.



Saif Al Islam, baada ya kuhofiwa kufa ameibuka na kutaka kuongoza Walibya. **PICHA: MTANDAO**

### ALIA LIBYA HAINA KITU

'Libya inavuja hakuna pesa wala usalama' ni maelezo ya Islam, ambaye alionekana baada ya miaka mingi, akisema "Sasa ni wakati wa kurudi nyumbani nchi inaangamia ... hakuna pesa, hakuna usalama. Hakuna maisha." Anasema Bin Gaddafi katika mahojiano hayo na kuongeza kuwa kwa sasa yeye ni mtu huru na anajiandaa kurudi tena katika siasa na kwamba watu ambao walikuwa wamemfunga jela hapo awali sasa wamekuwa 'marafiki' zake.

### ATAKUBALIWA LIBYA?

Hata hivyo, kurudi kwa Islam nchini Libya hakutakuwa rahisi. Sio tu kwamba anakabiliwa na shutuma za uhalifu wa kivita dhidi ya binadamu katika Mahakama ya Kimataifa ya Uhalifu (ICC), iliyoko The Hague Uholanzi, lakini pia anasubiriwa na hukumu ya mahakama moja ya Tripoli.

> Bin Gaddafi anadaiwa kuhusika na uhalifu wa kivita na kwa hivyo Mahakama ya Kimataifa ya Uhalifu (ICC) pia ilikuwa ikimtafuta.

The New York Times, iliandika kwamba licha ya haya yote, mtoto wa Muammar Gaddafi Seif al-Islam anaonekana kuwa 'thabiti'.

"Nina hakika masuala haya ya kisheria yanaweza kutatuliwa ikiwa watu wa Libya watanichagua kuwa kiongozi wao," anasema na kuongeza:"Nimekuwa mbali na watu wa Libya kwa miaka 10. Ili kurudi, nitalazimika kufanya kazi polepole kama mcheza dansi anayeitikia mirindimo ya muziki. Kucheza na akili za watu kidogo."

### HISTORIA YA KUKIMBIA

Mwaka 2011, wakati akikimbia kuokoa maisha yake, hakuona ni ajabu kujificha katika nyumba za watu nchini Libya, gazeti hilo linauliza.

Kujibu swali hili, Islam anasema, "sisi ni kama samaki na watu wa Libya ni bahari yetu. Bila wao tutakufa. Tunapata msaada kutoka kwao. Tunajificha hapa na kupigana hapa." Watu wa Libya ni bahari zetu. "

### ALIJIFICHA WAPI?

Saif Al Islam alikuwa wapi hadi sasa ni suala ambalo mchumi huyo mwenye Shahada ya PhD kutoka Shule ya London School of Economics, pengine atalitolea maelezo.

Hadi sasa hakuna habari kamili juu ya mahali alipokuwa kwa miaka kadhaa iliyopita licha ya kwamba sasa anaelekea kutangaza nia ya kuingia ikulu.

Bin Gaddafi anadaiwa kuhusika na uhalifu wa kivita na kwa hivyo Mahakama ya Kimataifa ya Uhalifu (ICC) pia ilikuwa ikimtafuta.

Alikuwa akikimbia kwa karibu miezi mitatu baada ya waasi kuchukua udhibiti wa Tripoli Agosti 2011, lakini akakamatwa na kufungwa na waasi hao.

Muammar Gaddafi na familia yake walikuwa madarakani nchini Libya kwa karibu miongo minne, lakini baada ya mapinduzi ya umma mwaka huo waasi waliondoa madarakani.

Katika machafuko hayo, waasi walichukua udhibiti wa mji mkuu Tripoli, na kisha Gaddafi akauawa .

Yapo madai kuwa watoto saba wa kiume wa Gaddafi pia waliuawa katika kipindi cha uasi , lakini Islam kutoroka na kunusurika.

Kabla ya mahojiano haya, Saif al-Islam alionekana mara ya mwisho mwaka 2014 kwenye video akiwa katika mji wa Xintan kwenye kesi yake iliyokuwa ikifanyika katika mahakama moja ya Tripoli.

### UASI/KIFO CHA GADDAFI

Muamar Gaddafi, alichukua uongozi mwaka 1969 katika mapinduzi yaliyomuondoa madarakani Mfalme Mohamed Sanusi.

Katika miaka yake ya kwanza baada ya kuchukua madaraka kwenye mapinduzi yasiyo na umwagaji wa damu, alikuwa kila walichohitaji Walibya.

Alikuwa na itikadi za kijamaa na anaelezwa kuwa alikuwa mfuasi mkubwa wa Rais wa zamani wa Misri Gamal Abdel Nasser.

Gaddafi alijipandisha cheo kutoka kapteni hadi kanali baada ya mapinduzi na kusimamia mafuta kikamilifu ili kuujenga uchumi wa Libya.

Akiba kubwa ya mafuta ilikuwa imegunduliwa nchini Libya mwishoni mwa miaka ya 1950, lakini uchimbaji huo ulidhibitiwa na kampuni za kigeni za mafuta, ambazo zilipanga bei kwa faida ya watumiaji wao wa nyumbani na kufaidika na nusu ya mapato.

Gaddafi alitaka kujadiliwa tena kwa mikataba hiyo, na kutishia kufunga uzalishaji ikiwa kampuni za mafuta zitakataa.

### KIFO CHA GADDAFI

Bila kudhibitiwa Gaddafi alipeleka kampeni yake ya kupinga ubeberu duniani kote, kufadhili na kusaidia vikundi vya wapiganaji na harakati za wapinzani popote alipowapata.

Alilenga pia wahamiaji wa Libya, kadhaa ambao waliuawa na vikosi vya mtandao wa majasusi wa Libya.

Hata hivyo, wakati wimbi la mapinduzi lililoanza kuvuma katika ulimwengu wa Kiarabu kutoka Tunisia mnamo Desemba 2010, Libya haikuwa juu ya orodha ya watu wengi wa "nani ajaye". Gaddafi kufikia wakati huo alikuwa ameshatambulika kama mtawala wa kimabavu ambaye alivumiliwa kwa miaka na raia. Lakini hakutambuliwa sana kama kibaraka wa magharibi kama viongozi wengine wa Kiarabu, walioshutumiwa kwa kuweka masilahi ya nje mbele ya yale ya ya watu wao.

Walibya walianza kunung'unikia ukandamizaji wapinzani, yakazuka maandamano dhidi ya utawala wake mwaka wa 2011.

Maandamano hayo yaligeuka na kuwa vita vya wenyewe kwa wenyewe huku Gaddafi akiapa kuwa hangetoroka nchi yake lakini shambulizi la NATO lililenga msafara wake, akamatwa na kundi la wapiganaji waliokuwa wakipambana na wanajeshi wake na kuuliwa.

**BBC.**





# Mbunge awaasa wanaokwepa chanjo Uviko-19

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

MBUNGE wa Viti Maalum (CHADEMA), Conchesta Rwamlaza, amewaasa Watanzania waliopo kwenye makundi ya kipaumbele kwenye chanjo ya Uviko-19 kuacha kujificha ili kujikinga na maambukizo ya ugonjwa wa corona.

Rwamlaza alitoa rai hiyo jana baada ya kupata chanjo hiyo katika Kituo cha Afya Bunge jijini hapa.

Alisema hakuna haja ya watu hao kujificha kwa kuwa elimu imetolewa na wataalamu ya umuhimu wa kupata chanjo hiyo.

"Wale wenzetu waliopo kwenye makundi ya kupata chanjo wasijifiche kwa kufuata maneno ya kutishwa wanatakiwa watambue afya zao ni bora kuliko maneno yanayopotoshwa na kuwakatisha tamaa," alisema.

Aliwahimiza Watanzania kuondokana na hofu ya kuchanjwa na kuwapuuza wanaobeza badala yake wachangamkie fursa hiyo muhimu ya kujikinga corona.

"Watanzania tujiepushe na watu ambao wanazusha na kupotosha kuwa chanjo hiyo ina madhara tena ni mbaya wakati serikali imethibitisha kuwa iko salama kwa ajili ya kujikinga na ugonjwa huo," alisema.

"Mimi nimechanja japo siyo lazima, lakini ni vyema kuwa balozi unayetetea afya yako sina uhakika kama anaweza kutokea mtawala anayefikiria kuliangamiza taifa analoliongoza la watu wake."

"Nimefuatilia sana juu ya chanjo nimekuwa nikifuatilia hata mataifa mbalimbali ya Ulaya watu wamepata chanjo na wako vizuri hata kama yapo maudhi madogo madogo hayo ni mambo ya kawaida ambayo hata wataalamu wa afya wameyatolea ufafanuzi."

Alishauri serikali kwa kupitia wataalamu wa afya kuendelea kutoa elimu katika makundi mbalimbali ikiwa ni pamoja na vijijini ambako pia huduma hiyo inatakiwa kuwafikia tena kwa wakati.

Alisema bado kuna ulazima wa serikali kuhakikisha elimu kwanza inapelekwa kwa watu wanaoishi vijijini ambao walio wengi ni wakulima ili wapate huduma hiyo ya chanjo.

"Hii itasaidia kuondokana na imani iliyokuwa imejengeka huko nyuma ya watu kuwa hakuna ugonjwa huo na kusababisha kupuuzwa, lakini ni ukweli usiopingika kuwa bado hali siyo salama na kujiamini bila kujilinda," alisema.

# Bodi yatakiwa kufanya tathmini kabla mikopo

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

BODI ya Mikopo ya Halmashauri imeagizwa kufanya tathmini ya kina kabla ya kutoa mikopo ili kufikia tija iliyokusudiwa.

Naibu Katibu Mkuu wa Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, anayeshughulikia elimu, Gerald Mweli, alitoa kauli hiyo jana alipofanya ziara na kuzungumza na viongozi wa bodi hiyo.

Alisema watendaji wa bodi hiyo wanatakiwa kubadili mtazamo wa kiutendaji na kuja na mawazo mbadala kwenye kuiendesha.

"Pamoja na mimi kujua changamoto zinazowakabili, lakini mnachotakiwa sasa mbadilike na mfanye kazi kwa matokeo, wakati wa uchambuzi wa bajeti tutumie fursa hiyo kuzipima halmashauri zile zinazoweza kufanya marejesho na ambazo zinasuasua katika marejesho."

"Lazima bodi iwe na ajenda, je, fedha zinazokopeshwa kwa halmashauri, mradi husika utaweza kurejesha fedha iliyokopewa?" Alihoji.

Hata hivyo, aliitaka bodi hiyo kubadili mfumo wa kudai madeni kwa halmashauri na kuwataka kufanyia kazi yale yaliyo ndani ya uwezo wao na yanayohitaji uamuzi wa wizara yafikishwe wizarani kwa hatua muhimu.

Awali, akisoma taarifa ya utendaji kazi wa bodi hiyo, Kaimu Mtendaji Mkuu wa Bodi hiyo, Yeremia Mahinya, alisema iliundwa chini ya Sheria ya Fedha ya Serikali za Mitaa, Sura ya 290 ya mwaka 2002, chini ya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa na inaendesha shughuli zake kwa matakwa ya sheria hiyo.

Alimweleza Naibu Katibu Mkuu huyo dhumuni la Bodi hiyo ni kuziwezesha Mamlaka za Serikali za Mitaa, kufanikisha miradi ya maendeleo itakayowasaidia katika kuinua mapato na kuchochea shughuli za kiuchumi.




Meneja wa kampuni ya utengenezaji na uuzaji wa vifaa vya kiasili kutoka nchi ya Burundi, Bibina Kampimbare Ange, akipanga bidhaa zake, katika Maonyesho ya Wajasiriamali ya Nanenane yanayoendelea kwenye viwanja vya Nyerere Square, jijini Dodoma jana. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# Wajasiriamali watakiwa kuchangamkia fursa

**Na Augusta Njoji,** BAHI

MKUU wa Wilaya ya Bahi, Mwanahamisi Munkunda, amewataka wajasiriamali wa vijiji vilivyopo katika Barabara Kuu ya Dodoma kwenda Singida kuchangamkia fursa za kibiashara ili kujiinua kiuchumi.

Munkunda aliyasema hayo jana wilayani humo alipokuwa akifungua mafunzo ya siku tatu ya kilimo na ujasiriamali yanayoratibiwa na Kanisa la Free Pentecost Tanzania (FPCT), kupitia mradi wa Tunandoto Tanzania Program Arusha, wenye lengo la kuiwezesha jamii kujiongezea kipato.

Alisema wananchi wa vijiji vya Uhelela, Nagulo, Bahi, Bahi Sokoni, Mpamantwa na Ibihwa ambao wanapitiwa na barabara hiyo hawatumii fursa ya ujasiriamali wa kuuza bidhaa wanazozalisha ikiwamo mchele, mboga na matunda.

"Niwashukuru viongozi wa Kanisa la FPCT kwa kushirikiana na halmashauri kuja na mradi wa Tunandoto Tanzania wenye lengo la kuiwezesha jamii hasa wajasiriamali kutambua fursa katika maeneo yao ili kuinua kipato chao," alisema.

Alisema mradi huo utawaongezea kipato wananchi kupitia kilimo bora na ujasiriamali kwa njia ya vikundi. Naye Mratibu wa Mradi huo, Lomayani Laizer, alisema tangu kuanzishwa kwa mradi huo mwaka 2014, Watanzania zaidi ya 100,000 katika mikoa mbalimbali nchini wamehudumiwa.

Alisema Watanzania zaidi ya 6,000 wamenufaika na mafunzo yanayotolewa na mradi na kipato chao kimeongezeka kupitia mavuno na mauzo ya bidhaa wanazozalisha.

Alibainisha kuwa kupitia mafunzo hayo na kwa kushirikiana na wataalamu wa halmashauri anaamini wajasiriamali hao na wananchi wengine kwa ujumla watatumia fursa zilizopo Bahi kujiongezea kipato.

Kwa upande wake, Ofisa Maendeleo ya Jamii wilayani humo, Denis Komba, aliahidi halmashauri hiyo itaendelea kutoa ushirikiano kwa kanisa hilo na kuziomba taasisi nyingine nchini kwenda Bahi kuwekeza na kuvijengea uwezo vikundi mbalimbali ili kujiongezea kipato.



# Serikali yatoa mablanketi 2,400 kukabili maafa

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

OFISI ya Waziri Mkuu Kitengo cha Maafa, imeukabidhi Mkoa wa Mbeya mablanketi 2,456 kwa ajili ya kusaidia wananchi watakaopata maafa kwenye mikoa yote ya Kanda ya Nyanda za Juu Kusini.

Mratibu wa maafa wa Mkoa wa Mbeya, Daniel Mwakitalu, aliyasema hayo juzi alipokuwa anapokea mablanketi hayo ambapo alisema vifaa hivyo ni sehemu ya serikali kuimarisha kitengo cha maafa kwenye maeneo mbalimbali.

Alisema mablanketi hayo ni sehemu ya msaada ambao serikali iliupata kutoka Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Watoto (UNICEF) na kwamba mablanketi hayo pamoja na vifaa vingine vitahifadhiwa kwenye ghala la maafa la kanda lililopo katika Kata ya Ituha jijini Mbeya. "Tumepokea marobota 136 ya mablanketi haya pamoja na vipande nane, wananchi wakipata maafa kwenye mkoa wowote, viongozi wanawasilisha barua na nyaraka zingine muhimu kwa Waziri Mkuu ili ofisi yake iidhinishe msaada wa vifaa hivi na sisi tunavipeleka kwa wahusika kulingana na maelekezo," alisema Mwakitalu.

Mwakitalu ambaye ni mchumi wa Mkoa wa Mbeya, alisema mbali na mablanketi hayo pia ghala hilo limesheheni vifaa mbalimbali vilivyohifadhiwa yakiwamo mahema, ndoo, masufuria, magodoro pamoja na vidumu vya kuchotea maji.

Alisema mikoa inayohusika kwenye Kanda hiyo ni Mbeya, Iringa, Ruvuma, Njombe, Songwe, Rukwa na Katavi na kwamba maafa yanayohesabika sana ni mafuriko, vimbunga, njaa na jua kali.

Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera, aliwataka wananchi wa mikoa yote ya ukanda huo kutoa taarifa mapema kila maafa yanapotokea ili taarifa zao zifike mapema katika Ofisi ya Waziri Mkuu na idhini ya kusaidiwa itolewe mapema.

Alisema serikali inaimarisha kitengo cha maafa ili kuhakikisha wananchi wanapunguziwa machungu baada ya kupata maafa ili badala ya kuendelea kuhangaika namna ya kuvipata waendelee na shughuli zao za uzalishaji.

Homera alisema hivi karibuni baadhi ya Halmashauri za Mkoa wa Mbeya zilinufaika na kitengo hicho cha maafa baada ya kukumbwa na mafuriko ambazo ni Halmashauri ya Wilaya ya Kyela na Halmashauri ya Busokelo wilayani Rungwe.

"Tunachoomba ni kwamba wananchi wawe wanatoa taarifa za ukweli kuhusu maafa yanayotokea, siyo tunaletewa taarifa za kuomba msaada kwamba kuna maafa sehemu kumbe sio za kweli, kitengo hiki kipo kwa ajili ya kuwasaidia Watanzania wote," alisema Homera.

Hata hivyo, alisema mablanketi hayo waliyoyapokea ni bora na yamethibitishwa ubora wake na Shirika la Viwango nchini na hivyo akawatoa hofu wananchi ambao wamekuwa wakiwa na wasiwasi na vitu vya misaada.

Aliwatahadharisha watu ambao wamekuwa wakitoa taarifa za upotoshaji kuhusu misaada ya kutoka nje ya nchi akidai kuwa upotoshaji huo unaweza ukazua hofu miongoni mwa wananchi.

Mwaka huu mafuriko yalitokea katika maeneo mbalimbali ya mikoa ya Nyanda za Juu Kusini hasa Mbeya na Rukwa ambapo wananchi walipoteza mali zao na kupata msaada kutoka katika kitengo hicho cha maafa.



Baadhi ya wakazi wa Kata ya Itezi jijini Mbeya, wakipita kwa shida kwenye barabara ya Itezi- Stendi ya Usangu jana, baada ya Wakala wa Barabara za Mjini na Vijijini (TARURA) kufunga kwa kuegesha moja ya mitambo kwa muda mrefu kuashiria kuendelea kwa kazi. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Wamiliki vyombo vya habari, COSOTA watofautiana

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

UMEIBUKA mvutano kati ya wamiliki wa vyombo vya habari wa mikoa ya Kanda ya Nyanda za Juu Kusini na Taasisi ya Hakimiliki (COSOTA) kuhusu viwango vya tozo za mirabaha kwa ajili ya kuwalipa wanamuziki kutokana na vyombo hivyo kutumia kazi za wasanii hao.

Mvutano huo uliibuka juzi jijini Mbeya wakati wa mkutano kati ya wamiliki wa vyombo vya habari, maofisa wa COSOTA na maofisa wa Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) Kanda ya Nyanda za Juu Kusini ambapo wamiliki walikuwa wanapinga viwango vya tozo.

Mkutano huo ulilenga kukusanya maoni ya wadau kuhusu viwango vya tozo hizo baada ya vya awali kutokubalika na kuleta matatizo, hali iliyomfanya Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Innocent Bashingwa, kuielekeza COSOTA kurudi kwa wadau kwenda kupata maoni ili vitolewe viwango vipya.

Mmoja wa wawakilishi wa wamiki wa vyombo vya habari, Isaya Mmbaya, alisema ili kufikia mwafaka wa viwango halisi ambavyo vyombo vya habari vinatakiwa kulipa, inatakiwa kuwe na mjadara kati ya wamiliki wa vyombo vya habari, COSOTA, TCRA na wasanii.

Alisema kwa sasa wamiliki wa vyombo vya habari wanashindwa kuamini kwamba viwango vinavyotajwa na COSOTA ndiyo mahitaji halisi ya wasanii na kwamba viwango vyenyewe ni vikubwa kuliko uhalisia.

Alisema kwa sasa wamiliki wa vyombo vya habari wanatakiwa kulipa Sh. 1,000,000 kiwango ambacho alidai kitasababisha baadhi ya vyombo vya habari kushindwa kujiendesha kutokana na gharama kuongezeka.

"Sisi hatukatai kulipa mirabaha, ila tunahitaji tukutanishwe na wasanii kupitia Taasisi ya maudhui Braza la Sanaa (BASATA) ili tujadiliane viwango sahihi, kwa sasa huu mjadara haufai kwa sababu COSOTA mmegeuka kuwa wasemaji wa wasanii," alisema Mmbaya.

Naye Gabriel Mbwile alisema COSOTA haijawashirikisha wamiliki wa vyombo vya habari kuhusu viwango wa tozo za awali ambazo walikuwa wanachangia Sh. 300,000 lakini wanataka kupandisha viwango.

Alisema hakuna taarifa zinazoonyesha idadi ya wasanii waliolipwa fedha zilizokusanywa kwenye vyombo vya habari pamoja na idadi ya wasanii waliojisajili COSOTA, hivyo akadai kuwa kuna uwezekano kukawa na udanganyifu.

Mbwile alisema endapo serikali itaridhia viwango vinavyopendekezwa na COSOTA, kuna uwezekano ikapoteza mapato mengi kutokana na wamiliki wengi wa vyombo vya habari kuamua kufunga vituo vyao na hata watakaoendelea wakaacha kupiga nyimbo ili kukwepa tozo hizo.

"Hizi tozo zitakuja kuleta matatizo mbele ya safari, waziri aliwataka mrudi kwetu baada ya kuona hivyo viwango vyenu vinatuumiza lakini ninyi badala ya kuondoa tatizo mnaongeza tatizo, mimi napendekeza bora tunaki na kiwango kilekile cha shilingi 300,000," alisema Mbwile.

Awali akitoa taarifa kuhusu tozo hizo, Mwakilishi wa COSOTA, Lupakisyo Mwambinga, alisema tozo hizo zilianzishwa kwa mujibu wa sheria za bunge kwa lengo la kuwasaidia wasanii kunufaika na kazi zao za kibunifu kama ilivyo kwa makundi mengine.

Alisema COSOTA imepewa mamlaka kisheria kukusanya mirabaha hiyo na kuigawa kwa wasanii na kwamba jambo hilo halifanyiki kwa Tanzania pekee bali hata katika mataifa mengine duniani yakiwamo ya Afrika Mashariki.

"Kinachotakiwa ni wamiliki wa vyombo vya habari kutoa maoni yenu kuhusu viwango mnavyoona vitakuwa rafiki, msipotoa maoni yenu kuna watu watapendekeza viwango kwa niaba yenu maana ni lazima hii mirabaha iwepo," alisema Mwambinga.

# Mil. 500/- kujenga barabara kutoka Chimala - Kapunga

**Na Nebart Msokwa,** MBARALI

SERIKALI wilayani Mbarali, imesema imepokea Sh. milioni 500 kwa ajili ya ujenzi wa barabara ya Chimala-Kapunga yenye urefu wa kilomita 26 ikiwa ni harakati za kuboresha miundombinu kwa ajili ya usafirishaji wa mazao ya wakulima.

Mkuu wa Wilaya ya Mbarali, Reuben Mfune, aliyasema hayo juzi alipozungumza na Nipashe kuhusu utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo wilayani humo ambapo alisema barabara hiyo ni muhimu kwa wakulima.

Alisema eneo la Kapunga ni miongoni mwa maeneo yenye wawekezaji wakubwa yakiwamo mashamba makubwa ya Kapunga Estate na wakulima wadogo, hivyo barabara hiyo ni muhimu.

"Kwa muda mrefu wananchi walikuwa wanaahidiwa kwamba barabara hii itaboreshwa, sasa tumeshapokea fedha hizi na tumeshatoa maelekezo kwa maofisa wa Wakala wa Barabara za Mijini na Vijijini (TARURA) ili waanze kuijenga," alisema Mfune.

Aliwataka wananchi kutoa ushirikiano kwa serikali ikiwamo kulinda vifaa vitakavyotumika kwenye ujenzi wa mradi huo ili visiibiwe pamoja na kukubali kupisha mradi huo kwa wale ambao watalazimika kuhamishwa.

Vilevile, alisema halmashauri hiyo imepokea Sh. milioni 500 kwa ajili ya ujenzi wa wodi tatu za wagonjwa kwenye Hospitali ya Wilaya inayojengwa katika eneo la Rujewa ili kuboresha huduma za afya kwa wananchi.

Vilevile alisema wanaendelea kushirikiana na wananchi kwenye ujenzi wa vyumba vya madarasa 127, ili kukabiliana na uhaba wa vyumba vya madarasa kwa ajili ya wanafunzi wa kidato cha kwanza wanaotarajia kuanza masomo Januari mwakani.



## Zanzibar yafafanua chanjo kipindupindu

**Na Rahma Suleiman,** ZANZBAR

WIZARA ya Afya, Ustawi wa Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto imesema chanjo ya kipindupindu inayoendelea kutolewa Zanzibar haihusiani na chanjo ya corona.

Hayo yalisemwa jana na Msimamizi wa Chanjo ya Kipindupindu Zanzibar, Dk. Fadhil Mohammed Abdallah, kupitia kitengo cha elimu ya afya Zanzibar wakati akizungumza na waandishi wa habari kuhusu awamu ya pili ya chanjo ya kipindupindu.

Dk. Fadhil aliwataka wananchi waliopata chanjo ya kipindupindu awamu ya kwanza kujitokeza kupata chanjo awamu ya pili ili kukamilisha dozi.

Aliwataka wananchi kuachana na kasumba zinazohusisha chanjo hiyo ni ya corona jambo ambalo si la kweli.

Sambamba na hayo, alisema lengo kuu ni kuunga mkono utekelezaji wa Mkakati wa Kutokomeza Kipindupindu Zanzibar (ZACCEP) wa mwaka 2018-2027, kuimarisha afya za wanajamii ili kushiriki kikamilifu katika shughuli za kujenga uchumi.

Naye Mkuu wa Kitengo cha Afya Zanzibar, Halima Khamis Ali, alisema awamu ya pili ya chanjo ya kipindupindu imeanza Agosti 8, mwaka huu, na mwananchi atakayepatiwa ni yule aliyepatiwa chanjo hiyo awamu ya kwanza.

Aidha, alisema mwananchi atakayekwenda kupatiwa chanjo hiyo ni vyema kwenda na utambulisho wa kupata chanjo awamu ya mwanzo ili kukamilisha chanjo ya awamu ya pili.

Pia alisema ni vyema kwa wananchi wakaendelea kufuata kanuni na taratibu za kinga ya kipindupindu ikiwamo ya kunawa mikono kwa maji tiririka na sabuni, kuchemsha maji ya kunywa, kunywa majisafi na salama, kufunika vyakula ili kuzuia nzi pamoja na kuosha matunda na mboga zinazoliwa bila kupikwa.

Alisema kwa awamu ya kwanza imefanyika vizuri na wananchi waliojitokeza katika shehia zilizopangwa ambapo limefikia asilimia 93.5.

Kutokana na mafanikio hayo, aliwataka waandishi wa habari kuendelea kuwahamasisha wanajamii kushiriki katika zoezi la chanjo dozi ya pili ili kufikia ufanisi na lengo la kutokomeza kipindupindu Zanzibar sambamba na kuwatoa hofu wananchi juu ya chanzo ya pili ya kipindupindu.

# Hemed ataka utatuzi ukosefu wa vifaa tiba

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MAKAMU wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Hemed Suleiman Abdulla, ameutaka uongozi wa Wizara ya Afya kutatua tatizo la ukosefu wa vifaa tiba katika hospitali na vituo vya afya ili kurahisisha upatikanaji wa huduma bora kwa wananchi.

Hemed alisema hayo jana wakati wa ziara ya kushtukiza aliyoifanya katika Hospitali ya Wazazi Mwembeladu na Hospitali ya Wagonjwa wa Akili Kidongo Chekundu kwa lengo la kujionea huduma zinavyotolewa kwa wananchi wanaofika katika hospitali hizo.

Alisema viongozi wenye dhamana ya kusimamia vituo vya afya wana jukumu la kuhakikisha vifaa tiba vinavyohitajika vinapatikana kwa wakati sambamba na kufanya ukarabati wa maeneo mbalimbali ili kuweka mazingira bora kwa wafanyakazi wanaotoa huduma kwa wananchi.

Katika Hospitali ya Mwembeladu, Makamu wa Pili wa Rais alisema maeneo ya kufanyia kazi kwa madaktari katika hospitali hiyo si ya kuridhisha, hivyo amemwagiza Mkurugenzi Mtendaji wa Hospitali ya Mnazi Mmoja, Dk. Msafiri Marijani, kuchukua hatua za haraka kwa kufanya ukarabati wa kawaida katika baadhi ya maeneo.

Akikagua sehemu ya kuhifadhia dawa na vifaa tiba, Hemed alimwelekeza Dk. Marijani kuhakikisha vifaa tiba ikiwamo mikoba ya kujifungulia na dawa muhimu zinazopatikana katika bohari kuu ya serikali, vinapatikana kwa wakati katika hospitali hizo.

Wafanyakazi wa hospitali hiyo walimwomba Hemed akiwa mtendaji mkuu wa shughuli za serikali, kuzipatia ufumbuzi kero zinazowakabili ikiwamo uchakavu wa jengo pamoja na upungufu wa wafanyakazi kwa ajili ya kutoa huduma katika chumba cha upasuaji.

Baada ya kukamilisha ziara yake katika hospitali hiyo, Makamu wa Pili wa Rais alitoa fursa kwa wananchi waliofika kupata huduma hospitalini hapo kuelezea changamoto wanazokabiliana nazo.

Katika kutoa kero zao, walisema wamekuwa wakikabiliwa na tatizo la upatikanaji wa kipimo cha damu hali inayosababisha usumbufu kwa kugharamia fedha ili kupata kipimo hicho nje.

Baada ya kusikiliza kero hizo, Hemed alisema serikali imedhamiria kutatua kero katika sekta ya afya ili kuwapatia huduma bora wananchi.

Wakati huo huo, Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar alifika katika Hospitali ya Wagonjwa wa Akili ya Kidongo Chekundu na kukagua maeneo mbalimbali yanayotolewa huduma kwa wagonjwa.

Akiwa katika eneo hilo, Hemed alitembelea sehemu maalumu za kumpuzikia wagonjwa ili kujionea mazingira halisi na aliwaagiza wafanyakazi kuendelea kutoa huduma kwa walengwa na kutokata tamaa kutokana na kero wanazokabiliana nazo.

Pia alitembelea jengo jipya linalotarajiwa kutoa huduma kwa wagonjwa na kuitaka kampuni ya RANS kukamilisha ujenzi huo ili kutoa fursa ya kutumika kwa jengo hilo na hatimaye kutatua tatizo la ufinyu wa nafasi kwa wafanyakazi.



Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Hemed Suleiman Abdullah (kulia), akizungumza na watendaji wa kitengo cha huduma ya damu salama huko Amani Zanzibar alipofanya ziara jana. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Wabainisha faida mradi kilimo mboga

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

UWAPO wa mradi wa viungo Zanzibar imeelezwa umeleta tija kubwa na kubadilisha maisha ya wanufaika kwa hatua ya awali kiwa umetimiza mwaka mmoja wa utekelezaji wake.

Kauli hiyo imetolewa na baadhi ya washiriki wa mkutano wenye lengo la kutazama fursa na changamoto za mradi huo kwa kipindi cha mwaka mmoja wa utekelezaji.

Akichangia mada katika mkutano huo, Bwana Shamba kutoka Wilaya ya Kaskazini B Unguja, Juma Kona Mosi, alisema mradi wa viungo umewawezesha wataalamu wa kilimo kufahamu kuwa kila sehemu inawezekana kufanya kilimo cha mboga na si kama walivyokuwa wakidhani awali kuwa kilimo hicho kinahitaji maeneo maalumu tu.

Alitolea mfano Shehia ya Donge Kiongwe, Mkoa wa Kaskazini Unguja kuwa miaka mingi wataalamu wa kilimo waliamini kuwa eneo hilo halifai kuanzisha kilimo cha mboga kutokana na ardhi yake kuwa ya mchanga lakini kuna mbinu mbalimbali ambazo zinawezesha kilimo hicho kufanya vizuri katika eneo hilo.

Pia alisema kupitia elimu waliyopatiwa na kisha kuwawezesha wakulima, hivi sasa ndani ya shehia hiyo kinamama wengi wanajihusisha na kilimo cha mboga na tayari wanavuna kila baada ya muda.

Sambamba na hilo alisema mabwana shamba walikuwa na sehemu zingine za kazi, hivyo hawakuwahi kufika kutokana na changamoto mbalimbali na waliamini kusingekuwa na haja ya kufika kutokana na wengi wao kukosa mwamko pamoja na kukata tamaa. Lakini hivi sasa, alisema watu wengi wamekuwa wakulima na wenye kupata faida kubwa.

Naye Khadija Msonda kutoka Shehia ya Mbaleni, alisema kabla ya ujio wa mradi wa viungo, walitumia nguvu nyingi kwenye kilimo kiasi kwamba baadhi walishindwa kutekeleza majukumu mengine ya msingi kwenye familia zao na wakati mwingine kusababisha hata ugomvi ndani ya ndoa.

Alisema ujio wa mradi huo umeleta faraja kubwa kwao na hivi sasa hawatumii muda mwingi kwenye kilimo lakini wanapata faida kubwa na kuwashirikisha wengine zaidi sambamba na kuepusha migogoro isiyo ya lazima ndani ya ndoa.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## NYUMBA ZINAUZWA

NYUMBA MBILI ENEO MOJA ZINAUZWA ZIPO UKONGA MOMBASA KWA DIWANI ,KUBWA INA VYUMBA VINNE VYA KULALA NA NYINGINE INA VYUMBA VITATU KILA CHUMBA NA SEBULE YAKE,MITA CHACHE KUTOKA BARABARA KUBWA,NI NYUMBA ZA KUPAUA,BEI MAELEWANO

**MAWASILIANO:** **0782 574669**
**0621 879477**


**OFISI ZA MATANGAZO MIKOCHENI INDUSTIAL AREA, PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 0782253676**


**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**

**USIMAMIZI WA MIRATHI FORM II**
**(S.M.M. 1984 NYONGEZA YA 5 KANUNI 2)**

**Katika mahakama ya mwanzo MJINI TANGA**

**Usimamizi wa mirathi 112 2021**

**Ombi la MUSSA HAMISI SHEKIMWERI kuteuliwa Msimamizi wa mirathi ya marehemu HUSSEIN HAMISI**

**Kwa YEYOTE ANAYEHUSIKA**

Watu wote wanaodaiwa kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu huyo wanaalikwa kuja na kuhudhuria kesi wakitaka mnamo tarehe 24/8/2021 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.
Wosia wa marehemu huyo upo mahakamani waweza kukaguliwa. Tarehe 4/8/2021

HAKIMU MKAZI
MAHAKAMA YA MWANZO
TANGA MJINI

1164401202

**UTAMBULISHO WA USIMAMIZI WA MIRATHI KATIKA**
**MAHAKAMA KUU YA TANZANIA**
**IRINGA**
**SHAURI NA.1/2021**
**MAOMBI YA BARUA YA USIMAMIZI WA MIRATHI YA**
**MAREHEMU……KENETH ELLY NYANGOYA**
**NA**
**WAOMBAJI…….1.SALOME DAUD WERE**
**2.OTIENO ELLY NYANGOYA**
**FOMU 58**
**TAARIFA YA KAWAIDA**
**(KANUNI 75)**

Watu wote wanaodai kuwa na haki katika mirathi ya marehemu aliyetajwa hapo juu wanafahamishwa kufika na kuangalia shauri hili katika jalada kama wanaona inafaa kabla ya kutolewa kwa barua ya usimamizi wa mirathi kwa waombaji waliotajwa hapo juu
Pingamizi kuhusu maombi haya yawe yameandikishwa mnamo au kabla ya **tarehe 12/08/2021**
Hati hii imetolewa kwa amri yangu na muhuri wa mahakama hii leo **tarehe 22/07/2021**

1164021102

## KUPOTEA KWA CHETI



**RAHELI TUMSIFU UROKI** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S0265/0015** kilichotolewa na baraza la mitihani kupitia shule ya secondary **CORNELIUS mwaka 2019,**yeyote atakayeiokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi
Polisi taarifa **MDL/K/B.1/1/VOL 1/107**

1164022202

## KUPOKELEWA NA KADI YA PIKIPIKI

**KAHAMA IMPORT AND EXPORT LTD**
Anatangaza kupokelewa na kadi ya pikipiki yenye namba za usajili **MC.220 BKE** yenye Engine no. **162FMLG00000007, Chassis no. LTZPCK-LN6G6200007** yenye rangi Nyekundu.
Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi kilichopo jirani yake.
Taarifa ya jeshi la polisi.
**KAH/TR/RB/398/ 2021.**

1164402402

## TAARIFA KWA UMMA

Rejea tangazo letu la tarehe **10.08.2021** katika gazeti la Nipashe kuhusu mnada wa hadhara. Mnatangaziwa kuwa kuna marekebisho ya tarehe kuwa **mnada utafanyika tarehe 18.08.2021 kuanzia saa nne Asubuhi na sio tarehe 24.08.2021** kama ilivyotangazwa hapo awali gazetini.
Tunaomba radhi kwa usumbufu uliojitokeza.
Mnada wa hadhara wa gari utafanyika **Makumbusho yard – DSM** mahali dhamana ilipo, Mnada utaendeshwa na **SEPCO Debt Collection & Auctioneering Co. Ltd** kwa idhini tuliyopewa na **Tujijenge Tanzania Ltd.** Gari ni mali ya MARY HARRIETH CHIBIBI LONGWAY /AMINA MARTIN BAGULE (Mkopaji) **Toyota land Cruiser T.297 ASV**

**Mawasiliano piga: -**
**SEPCO - 0715683777/0712670704**

1164402502

**KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA**
**WILAYA YA SAME.**
**LILILOPO SAME**
**MAOMBI MADOGO NA. 24 YA 2020**
**NEEMA OMARY KATAMBA………MWOMBAJI**
**DHIDI YA**
**ATHUMANI SENKONDO NA WENZAKE 10……………**
**MJIBU MAOMBI**

**KUITWA SHAURINI**
**KWA: SENKONDO MKULIA,MAVOO MKULIA,KIPESHA KATAMBA ,OMARI BAKARI,SENKONDO BAKARI, CHAKUINKWA KARIA,LEMNGA SENKORO,SENKORO RAMADHANI**
**POPOTE MLIPO**

**KWA KUWA** ,Mwombaji ameleta maombi yake na yameelezwa katika Baraza la Ardhi na Nyumba Wilaya ya Same . Shauri limepangwa kutajwa tarehe 03/09/2021 saa mbili na nusu (2:30) asubuhi mbele ya Mh. Mwenyekiti **T.J.WAGINE**
**HIVYO BASI ,** mnatakiwa kufika mahakamani ninyi wenyewe au mawakili wenu au mtu ambaye ameruhusiwa kisheria na kutakiwa kuleta utetezi wenu wa maandishi ndani ya siku 21 kuanzia tarehe ya Tangazo hili.
**ANGALIA :** Kama hutahudhuria tarehe iliyotajwa hapo juu, Mahakama itasikiliza shauri hili na kutoa uamuzi upande mmoja dhidi yenu .
**IMETOLEWA NA BARAZA HILI LEO TAREHE 29/07/ 2021.**

**MWENYEKITI**
**BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA LA WILAYA YA SAME**

1164402602

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**MOHAMED ADAM MEKI** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya **TOYOTA CHASER** yenye namba za usajili **T 809 CBT** chasis namba **GX1000105406** engine namba **1G6766932,** yeyote atakayeiokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi. Polisi taarifa **KIL/SAN/RB/384866/2021**

1164402702

**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**KATIKA MAHAKAMA YA HAKIMU MKAZI MWANZA**
**SHAURI LA MAOMBI NAMBA 01 YA MWAKA 2021**
**SABINA CHACHA……………………………MWOMBAJI**
**DHIDI YA**
**KASSIM ALLY & MWENZIE………WAJIBU MAOMBI**
**KWA: KASSIM ALLY**
**POPOTE ULIPO**

Mahakama hii inakufahamisha kwamba mwombaji amefungua maombi dhidi yenu nakala yake inapatikana katika mahakama hii. Shauri limepangwa kusikilizwa mnamo **tarehe 13/8/2021 saa 06:00 MCHANA** na unatakiwa kuwepo au kuwakilishwa kisheria pamoja na kuleta utetezi wako dhidi ya maombi haya .
Zingatia kwamba kutokufika kwako tarehe hiyo, shauri litaanza kusikilizwa bila ya wewe kuwepo, na maamuzi kutolewa.
Imetolewa leo hii mbele yangu na mhuri wa mahakama **tarehe 06/8/2021**

HAKIMU MKAZI MKUU
MWANZA

**HAKIMU MKAZI MKUU**
**MWANZA**

1164402802

## KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**MOSA HOLDING LIMITED**
ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA GARI AINA YA TRAILER YENYE NAMBA ZA USAJILI **T 208 BDX** YENYE CHASSIS NO **MT01016609**
KWA YEYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHOCHOTE CHA POLISI
TAARIFA YA POLISI
**KAH/ RB/400/2021**

1164403402

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**
**USIMAMIZI WA MIRATHI FORM II**
**(S.M.M. 1984 NYONGEZA YA 5 KANUNI 2)**
**KATIKA MAHAKAMA YA MWANZO MJINI TANGA**
**USIMAMIZI WA MIRATHI AFFL 11 2021**
**OMBI LA JUMA MUSSA HEMEDI KUPAZA**
**KUTEULIWA**
**MSIMAMIZI WA MIRATHI YA MAREHEMU MUSSA HEMEDI KUPAZA @ HUNGO HEMEDI KUPAZA**
**KWA YEYOTE ANAYEHUSIKA**

WATU WOTE WANAODAIWA KUWA NA UHUSIANO WOWOTE NA MIRATHI YA MAREHEMU HUYO WANAALIKWA KUJA NA KUHUDHURIA KESI WAKITAKA MNAMO TAREHE 31/8/2021 KABLA HUYO MWOMBAJI HAJATEULIWA KUWA MSIMAMIZI WA MIRATHI HIYO.
WOSIA WA MAREHEMU HUYO UPO MAHAKAMANI WAWEZA KUKAGULIWA .
**TAREHE 10/8/2021**

HAKIMU MKAZI
MAHAKAMA YA MWANZO
TANGA MJINI

1164403302

## KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**SARAH JOHN PONERA ANATANGAZA kupotelewa na kadi ya gari aina ya TOYOTA IPSUM yenye namba ya usajili T775 BNS chasis namba SXM107139134 injini namba 3S7935380 Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi taarifa ya polisi RB namba IRI/IRI/RB/299157/2021**

1164403202

## KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**HASSAN SELEMAN MTENGA anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya NISSAN CIVILIAN yenye namba za usajili T 362 DGW chasis namba BHW41010115 engine namba TD421626652,yeyote atakayeiokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi Polisi taarifab URA/RB/3532/204**

1164403102


**Kwa Habari Motomoto**

usikose Gazeti lako
la Nipashe kila siku
Tupigie
0782253676

Nipashe
MWANGA WA JAMII



**NJOO UTANGAZE BIDHAA YAKO KWA BEI NAFUU SANA**



TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji
THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

HABARI KIMATAIFA

# Nchi 6 Afrika zakithiri watoto kuugua Ukimwi

**New York,** MAREKANI

RIPOTI ya Umoja wa Mataifa (UN), imesema Nigeria, Msumbiji, Afrika Kusini, Tanzania, Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo (DRC) na Zambia zina idadi kubwa ya watoto waishio na Virusi Vya Ukimwi (VVU), na hawatumii dawa za kufubaza virusi.

Nchini Nigeria kuna idadi kubwa ya watoto walio na VVU, kati ya watoto watano, mmoja ameambukizwa virusi hivyo.

Kulingana na ripoti hiyo, inakadiriwa kwamba watoto 620,000 wanaoishi na VVU katika nchi 21 za Afrika, walikuwa hawapokei dawa za kupunguza makali ya virusi hivyo.

Inasema watoto katika Bara la Afrika wanatelekezwa linapokuja suala la matibabu yanayohusiana na Virusi Vya Ukimwi (VVU) na kwamba idadi kubwa ya watoto hao watafariki kabla ya kutimiza umri wa miaka miwili.

Shirika la Umoja wa Mataifa linaloshughulikia Ukimwi (UNAIDS), pamoja na washirika wake linaonya hatua zilizopigwa katika kuumaliza ugonjwa huo, miongoni mwa watoto wa hadi umri wa miaka 14, vijana na kinamama walio na umri mdogo, zimekwama.

**Ni nchi sita kati ya 21 zilizotoa dawa kwa watoto katika mwaka 2020, ambazo ni Kenya, Eswatini, Lesotho, Malawi, Namibia na Zimbabwe.**

UN, linasema kwa sasa, lengo halikutimizwa hata moja kwenye malengo yake ya mwaka 2020.

Kwa mara ya kwanza idadi ya watoto walio kwenye matibabu ya ugonjwa huo ilipungua.

Ni nchi sita kati ya 21 zilizotoa dawa kwa watoto katika mwaka 2020, ambazo ni Kenya, Eswatini, Lesotho, Malawi, Namibia na Zimbabwe.

Mkurugenzi wa Idara ya Mikakati ya UNAIDS, Peter Ghys, alisema upungufu uliyoko katika kuwatibu watoto ugonjwa huo duniani ni tatizo kubwa.

Takwimu zinaonyesha kwamba watu wazima ndio wanaopata matibabu zaidi ya watoto.

Ghys alisema kupungua kwa idadi ya watoto wanaopewa matibabu pia kumetokana na janga la virusi vya corona.

Alisema mifumo ya matibabu ni tofauti katika nchi mbalimbali na nchi zengine zilikuwa zimejihami vyema.

Nchi zilizo na mifumo duni ya matibabu zimeonekana kuwatelekeza watoto katika masuala ya matibabu ya virusi hivyo.

Mojawapo ya nchi zilizopambana vyema na matibabu ya watoto walio na ugonjwa huo ni Eswatini ambayo mkurugenzi huyo wa UNAIDS anasema, licha ya kuwa ni nchi ndogo, ina uwezo wa kuwatibu watoto na hata watu wazima.

Kwa upande mwingine, nchi zilizo na uwezo mdogo wa kimatibabu ni pamoja na Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo (DRC), Angola, Chad na Burundi.

Ghys alisema katika nchi hizo, kumekuwa na mchanganyiko wa sababu zilizosababisha matibabu miongoni mwa watoto yasitolewe ikiwamo, mifumo duni ya afya pamoja na masuala ya kisiasa kupewa kipaumbele.

Katika mahojiano na DW Ghys pia alisema kwamba imekuwa wazi kuwa katika miaka ya hivi karibuni, watoto wamekuwa hawapimwi VVU.

Ghys alisema watoto wanapozaliwa hawapimwi au wanapimwa, ila kuna upungufu katika mifumo na watoto hao hata wanapopatikana na maambukizi, hawaanzishiwi matibabu.

Ghys alisema ili kukabiliana na hali hiyo, hivi karibuni kumekuwa na mikakati mingine ya upimaji.

Ripoti hiyo ya UN inazidi kueleza kuwa, theluthi mbili ya maambukizi miongoni mwa watoto mwaka 2020 yalikuwa katika nchi sita ambazo ni Nigeria, Msumbiji, Afrika Kusini, Tanzania, DRC na Zambia, huku Nigeria ikiwa na idadi kubwa zaidi.

Katika mahojiano na DW, Thembisile Xulu, Mkurugenzi wa Baraza la Kitaifa la Ukimwi Afrika Kusini SANAC, alisema nchini humo, unyanyapaa bado ni tatizo kubwa na kizingiti katika juhudi za kupambana na HIV.

Xulu aliongeza kwamba Afrika Kusini kwa sasa inashughulikia njia kadhaa za kuhakikisha kwamba malengo ya matibabu yanafikiwa.

Alisema njia bunifu zinahitajika kuhakikisha kwamba watoto wadogo na vijana wanaendelea na mipango yao ya matibabu. **DW**

## Waasi Tigray wakana shambulio dhidi ya Hospitali

**Afar,** ETHIOPIA

WAASI wa Tigray wamekanusha kuhusika na shambulio kwenye kituo cha afya katika Jimbo la Afar huko Ethiopia, ambalo liliwaua watu wasiopungua 12.

Utawala wa Mkoa wa Afar unalaumu vikosi vya Tigray kwa shambulio hilo, wakati mapigano katika mzozo wa miezi tisa wa Ethiopia yakizidi hadi katika majimbo yanayopakana na Tigray.

Daktari katika Mkoa wa Afar aliiambia BBC kwamba watu hao 12 walifariki, kutokana na majeraha waliyoyapata katika shambulio kali la silaha katika Kituo cha Afya cha Galikoma.

Watu zaidi ya 30 wakiwamo wanawake na watoto walihitaji matibabu ya dharura baada ya shambulio hilo.

Msemaji wa Utawala wa Jimbo la Afar alisema raia wengi zaidi walifariki katika eneo la tukio, hakuweza kutoa idadi rasmi ya vifo.

Alilaumu vikosi vya Tigray, msemaji wa Tigray People's Liberation Front alisema kwenye Twitter kwamba ripoti za shambulio hilo ni la kutisha. Alikana kuhusika kwa kundi hilo na kusema wako tayari kushirikiana na uchunguzi wowote kubaini ukweli.

Kituo hicho cha afya kilitumika kuwahifadhi watu waliokimbia makazi yao na kuweka msaada wa chakula. **BBC**



Wakazi wa Kitongoji cha Thrakomakedones, Kaskazini mwa mji wa Athens nchini Ugiriki, wakiokoa mifugo yao juzi, baada ya moto wa msituni kusogea eneo hilo. **PICHA: REUTERS**

## Dunia yajadili joto la kutisha

**New York,** MAREKANI

VIONGOZI wa dunia, mashirika ya kutunza mazingira na washawishi, wamezungumzia kwa mchanganyiko wa mshtuko na hali ya matumaini katika ripoti ya kutisha iliyotolewa na wanasayansi wa Umoja wa Mataifa (UN), kuhusu mabadiliko ya tabianchi.

Mjumbe wa Marekani kuhusu tabianchi na ambaye ni Waziri wa zamani wa Mambo ya Kigeni, John Kerry, alisema ripoti hiyo ya jopo la IPCC, ambayo iliyonya kuwa dunia, inaelekea kufikia kiwango cha joto cha nyuzi 1.5 za celsius karibu mwaka wa 2030.

Alisema inaonyesha kuwa mgogoro wa tabianchi unaongezeka na kuwa mbaya zaidi.

Waziri Mkuu wa Uingereza, Boris Johnson, ambaye serikali yake itaandaa mkutano wa kilele wa UN kuhusu tabianchi mwezi Novemba, alisema tathmini hiyo ya wanasayansi inafungua macho. **DW**

# NUNO ATHIBITISHA KANE KUIVAA CITY




**LONDON,** England

HARRY Kane atapatikana katika mchezo wa kwanza wa Ligi Kuu ya England dhidi ya Manchester City Jumapili, kocha Nuno Espirito Santo amedokeza.

City waliripotiwa kuwasilisha mezani dau la pauni milioni 100 kwa mshambuliaji huyo ambaye alikataliwa, ingawa mabingwa hao wa Ligi Kuu bado wana nia naye.

Nuno siku ya Jumatatu alikuwa kwenye mazungumzo na nahodha huyo wa England, ambaye mabao yake 23 katika msimu uliopita yalimfanya kufanikiwa kupata tuzo yake ya tatu ya Kiatu cha Dhahabu, kabla ya kupendekeza Kane aweze kushiriki dhidi ya vijana wa Pep Guardiola.

Alipoulizwa juu ya kupatikana kwa mchezaji huyo kwenye mchezo wa City, Nuno aliiambia Sky Sports: "Wachezaji wote kwenye kikosi ambacho hucheza kila siku watakuwa chaguo kwetu, basi ni juu yetu kuamua."

Guardiola amekuwa akikata tamaa wakati wa kumtafuta Kane, akisisitiza nia yake kwa mshambuliaji huyo Ijumaa iliyopita licha ya kuwa tayari amempata Jack Grealish kwa ada ya kuvunja rekodi ya pauni milioni 100.

Endapo Kane atajiunga na Grealish kama mchezaji wa City mwishoni mwa dirisha la uhamisho bado haionekani, lakini Nuno atakuwa na matumaini kuwa mchezaji wake anaweza kuanza kampeni na timu yake kwa ushindi.

# United yaachana na Trippier

**MANCHESTER,** England

MASHABIKI wa Manchester United wasitegemee kumwona Kieran Trippier akitua Old Trafford kwenye dirisha hili la usajili, hii ni kwa mujibu wa ripoti za usajili.

United wamekuwa wakihusishwa na Trippier tangu kufunguliwa kwa dirisha hili la usajili, kitu pekee ambacho kwa namna moja au nyingine kimekwamisha usajili huu ni dau kubwa la pauni milioni 43 lililowekwa na Atletico Madrid.

Ripoti mbalimbali za usajili zimedai kuwa, Man United imeamua kumbakiza Diogo Dalot kwenye kikosi chao na atapambania namba dhidi ya Aaron Wan-Bissaka kwa msimu huu.

Uamuzi wa kumbakiza Dalot, ni matokeo ya AC Milan kushindwa kufikia makubaliano ya kumsajili mchezaji huyo na badala yake, United wameona ni bora akabaki na kupambania namba yake kwenye kikosi cha Ole Gunnar Solskjaer kuliko kutoa fedha ndefu kwa Trippier.

Hii huenda ikawa ni habari njema kwa Arsenal ambao pia wanahusishwa na Trippier.

Endapo Atletico Madrid wataamua kutimiza azma ya mchezaji huyo kurejea England, pengine anaweza kutua pale kwenye dimba la Emirate.







# Pique: Barca imetetereka kuondoka kwa Messi

**BARCELONA,** Hispania

BEKI wa Barcelona, Gerard Pique, amesema wametetereka kidogo baada ya kuondoka kwa Lionel Messi, licha ya timu hiyo kutwaa taji la Joan Gamperna baada ya kuifunga Juventus mabao 3-0.

Ilikuwa jioni ya hisia huko Camp Nou, na mkutano na waandishi wa habari ulifanyika mapema siku ambayo Messi aliaga klabu hiyo akilia machozi.

Pique amekiri kuwa matumaini si makubwa kwa msimu ujao kutokana na kupoteza mmoja wa wachezaji wakubwa wa mchezo huo.

"Timu imetetereka kidogo kwa sababu ya kuondoka kwa Lionel Messi, tutapoteza ubunifu katika kushambulia, lakini tunapaswa kusonga mbele, mashabiki wanatarajia mengi kutoka kwetu," alisema akiwaambia waandishi wa habari.

"Tumepoteza mchezaji bora wa wakati wote. Imetuumiza na ilimuumiza pia. Sijui hadithi yote, pande mbili zimesema kwamba imekuwa suala la namba.

"Uongozi wa miaka ya mwisho haujasaidia, lakini historia inaonyesha kwamba tutasimama tena.

"Watu wanataka sana kuja uwanjani na lazima tufurahishe mashabiki. Lazima tuanze kushinda na kuwapa vitu vizuri. Tunahitaji mashabiki pamoja nasi," aliongeza Pique.

# James kuamua hatima yake Man United

**MANCHESTER,** England

WAKATI mashabiki wa Manchester United wakisubiri kuona msimu ujao unakwendaje, baadhi ya wachezaji wanamaamuzi ya kufanya, Daniel James ni mmoja wao.

James alijiunga na United mwaka 2019 akiwa miongoni mwa wachezaji watano wa kwanza kusajiliwa (akiwamo Harry Maguire, Aaron Wan-Bissaka, Bruno Fernandes na Odion Ighalo) kwenye uongozi wa kocha Ole Gunnar Solskjaer.

Maisha ndani ya United, yamekuwa ni safari ya kupanda na kushuka kwa James, hii imemfanya winga huyu kukosa namba ya kudumu kwenye kikosi cha timu hiyo.

Man United imekamilisha usajili wa Jadon Sancho, kuongezeka kwa winga huyu, kunaongeza ushindani wa nafasi kwenye kikosi hicho na huenda James akaathirika zaidi kwa kukosa namba kwa muda mrefu.

Ni dhahiri kuwa, James anahitaji kucheza mara kwa mara na kwa sababu hiyo, dirisha hili la usajili ni fursa pekee ya yeye kuondoka United.

Leicester City na Leeds United zinahusishwa na usajili wa winga huyu raia wa Wales.

Leeds United si wageni katika mbio za kuiwania sahihi ya James, walifanya hivyo msimu uliopita bila ya mafanikio.

Man United wameweka thamani yake kuwa ni pauni milioni 15 kwa timu yoyote inayomtaka winga huyo.




# ROMA YAKUBALI KUMSAJILI ABRAHAM



**ROME,** Italia

KLABU ya AS Roma ya Italia imekubali kumsajili mshambuliaji Tammy Abraham wa Chelsea kwa dau la pauni milioni 34.

Mshambuliaji huyo mwenye umri wa miaka 23, sasa ni lazima aamue iwapo anataka kujiunga na klabu hiyo ya Italia chini ya kocha Jose Mourinho.

Chelsea inataka kuuza wachezaji kadhaa ili iweze kupata pauni milioni 98 kumnunua Romelu Lukaku kutoka Inter Milan na mpango unaoendelea wa uhamisho wa beki wa Sevilla, Jules Kounde.

Abraham ambaye alifunga mabao 12 msimu uliopita, tayari amekataa uhamisho kwenda Atalanta ya Ligi Kuu Italia, Serie A, lakini anaeleweka kuwa anapenda kufanya kazi na kocha wa Roma, Mourinho.

Awali, nyota huyo wa England alikuwa akihusishwa na klabu kadhaa za Ligi Kuu England, lakini hakuna timu iliyotoa ofa.

Klabu za Arsenal, Liverpool ni miongoni mwa klabu ambazo zimekuwa zikitajwa kuwania saini ya mchezaji huyo.

# Stones alamba dili nono Man City

**MANCHESTER,** England

BAADA ya kuwa na msimu mzuri ndani ya Manchester City na timu ya Taifa ya England, John Stones, ameongezewa mkataba mpya ndani ya klabu hiyo.

Stones amepewa mkataba mpya wa miaka mitano kusalia hapo kwenye dimba la Etihad ikiwa ni sambamba na kupewa mshahara wa pauni 250,000 kwa wiki.

Mchezaji huyo aliitumikia City kwenye michezo 35 msimu uliopita akiisaidia timu hiyo kutwaa ubingwa wa Ligi Kuu England (EPL) na Kombe la Carabao.

Akiwa na timu ya Taifa ya England, Stones aliiongoza vema timu hiyo kwenye safu ya ulinzi katika mashindano ya Euro 2020 ambapo walipoteza mchezo wa fainali dhidi ya Italia.

Taarifa ya klabu hiyo ilisema imefikia makubaliano ya kumwongeza mkataba wa miaka mitano nyota huyo.



HABARI MICHEZO

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# BAYERN SASA KAZI MOJA TU KUMSAJILI HAALAND

●●● Mabao 60 katika michezo 60, lazima umzingatie, tuna nia ya dhati kutaka kumsajili...

**MUNICH,** Ujerumani

KLABU ya Bayern Munich imeelekeza nguvu zake kwa mshambuliaji kinda, Erling Haaland kutoka Borussia Dortmund, kwa mujibu wa Bild.

**Haaland amekuwa kwenye kiwango bora ndani ya Dortmund na barani Ulaya kwa ujumla.**

Uwezo wake wa kuzifumania nyavu, ni kitu ambacho kinawatoa udenda klabu nyingi duniani kwa sasa.

Chelsea walijaribu kujitosa msimu huu, lakini waliambulia patupu, na walihamia kwa Romelu Lukaku na wanatajwa kwamba wamefikia makubaliano ya kukamilisha usajili wa mshambuliaji huyo.

Klabu zilizobaki kuhusishwa na Haaland ni Manchester United na Real Madrid, lakini havikutoa ofa ya kumsajili kipindi hiki cha majira ya joto. Mkurugenzi wa Michezo wa Bayern Munich, Hasan Salihamidzic, amethibitisha kuwa klabu hiyo ya Ujerumani ina nia ya kumsajili mshambuliaji huyo wa Norway mwenye umri wa miaka 21.

"Ni mchezaji mzuri, na nimesikia ni kijana mzuri pia. Lazima umtupie jicho lakini ni mchezaji wa Dortmund,"

"Mabao 60 katika michezo 60, lazima umzingatie. Tuna nia ya dhati kutaka kumsajili." alisema Salihamidzic akinukuliwa na gazeti la Bild

Hata hivyo, ni suala gumu kwa Bayern Munich kupambania sahihi yake na baadhi ya klabu nyingine kubwa barani ulaya kwa sasa. Hii ni kutokana na hali ya uchumi wa klabu hiyo kwa sasa.

## ZISIKUPITE

### XHERDAN AWANIWA LYON

KLABU ya Lyon imeweka mezani ofa ya kupata huduma ya mshambuliaji wa Liverpool na Uswizi, Xherdan Shaqiri mwenye umri wamiaka 29. ***(L'Equipe - via Get French Football News)***

### UTD WAJIPAPASA KWA MESSI

HUENDA Manchester United inaandaa ofa ya kumjaribu mshambuliaji wa zamani wa Barcelona, Lionel Messi mwenye umri wa miaka 34, ili asihamie Paris St-Germain. ***(Daily Star)***

### PSG WAACHANA NA POGBA

KLABU ya PSG pia imehitimisha jithada zao kumsajili kiungo wa Manchester United na Ufaransa, Paul Pogba mwenye umri wa miaka 28. ***(Le Parisien)***

### LUKAKU SASA SAFI CHELSEA

BAADA ya kupita sehemu ya kwanza ya matibabu yake huko Chelsea, mshambuliaji wa Ubelgiji na Inter Milan, Romelu Lukaku mwenye umri wa miaka 28, anaweza kucheza kwenye mchezo wao wa ufunguzi wa Ligi Kuu England dhidi ya Crystal Palace Jumamosi. ***(Daily Star)***

### MESSI KUNG'OA 10 PSG

KLABU ya PSG wako tayari kuuza hadi wachezaji 10, pamoja na kiungo wa zamani wa Senegal, Idrissa Gueye mwenye umri wa miaka 31, ili kukamilisha usajili wa Lionel Messi. ***(Athletic)***

### VARANE KUTAMBULISHWA

MANCHESTER United iko tayari kuthibitisha kusainiwa kwa beki wa Real Madrid, Raphael Varane mwenye umri wa miaka 28, kwa wakati ili Mfaransa huyo aweze kucheza mchezo wa Ligi Kuu England Jumamosi dhidi ya Leeds. ***(Daily Star)***

### LIVERPOOL YAMTAKA DOKU

LIVERPOOL inaangalia uwezekano wa uhamisho wa winga wa Rennes na Ubelgiji, Jeremy Doku mwenye umri wa miaka 19. ***(Voetbal 24)***

### TAMMY AGOMBEWA ENGLAND

MSHAMBULIAJI wa Chelsea na England, Tammy Abraham mwenye umri wa miaka 23, analengwa na Arsenal, Roma na Atalanta. ***(Goal)***

### MOURINHO AMTAKA LACAZETTE

KOCHA wa AS Roma, Jose Mourinho, bado ana hamu ya kutaka kumsajili mshambuliaji wa Arsenal na Ufaransa, Alexander Lacazette mwenye umri wa miaka 30. ***(Gazzetta dello Sport - via Boot Room)***

### YAMUWANIA LINGARD

KLABU ya Leicester inataka kumsajili kiungo wa Manchester United, Jesse Lingard mwenye umri wa miaka 28, ikiwa Muingereza mwenzake James Maddison mwenye miaka 24, ataondoka klabuni humo. ***(Football London)***

# AUCHO NI BONGE LA MCHEZAJI - MAYANJA

Na Adam Fungamwango

KOCHA wa zamani wa klabu ya Simba, Jackson Mayanja, ameipongeza klabu ya Yanga kwa kupata mchezaji mzuri, Khalid Aucho huku akifafanua kuwa kiungo huyo atawasaidia sana kwenye michuano ya Ligi ya Mabingwa na Ligi Kuu Tanzania Bara.

**Mayanja ambaye alishawahi kuzifundisha klabu za Kagera Sugar, na Coastal Union, amempongeza pia mchezaji huyo kwa kupata timu nzuri na kubwa ambayo itamtangaza kimataifa pia.**

Akizungumza kutoka nchini Uganda, Mayanja ambaye ni nahodha wa zamani wa Uganda Cranes, amesema anataka kushuhudia vita ya Waganda wawili, Aucho na Thadeo Lwanga kwenye vikosi hivyo viwili hasimu nchini Tanzania.

"Ni mchezaji mzuri. Ana uzoefu na ana nguvu pia, Yanga imepata mchezaji mzuri na anaichezea timu ya Taifa ya Uganda. Nadhani watu wengi hasa Watanzania walimuona kwenye AFCON iliyopita na bado yupo timu ya taifa," alisema Mayanja.

Alisema uwapo wake kwenye kikosi cha Yanga utakuwa ni faida pia kwa timu yao ya taifa, kwani changamoto atakazokuwa akizipata, zitamfanya kuzidi kuongezeka ubora na kuisaidia nchi yao.

"Kwa sisi Waganda tunafarijika kwa sababu Lwanga yupo Simba na sasa Aucho atakuwa Yanga. Watakuwa wanaonyeshana ufundi. Na hii itakuwa si faida kwa timu hizo tu, bali hata kwa timu ya Taifa ya Uganda," alisema.

Juzi, Yanga ilimtambulisha kiungo mkabaji huyo ambaye ametokea klabu ya Lel Makkasa ya nchini Misri.

Kabla ya timu hiyo, alizichezea timu za Tusker na Gor Mahia za nchini Kenya mwaka 2015 mpaka 2016, na baadaye alijiunga na klabu ya Baroka FC ya Afrika Kusini mwaka 2016, kabla ya kwenda kujiunga na klabu ya Red Star Belgrade ya nchini Serbia 2017, lakini mwaka huo huo akatolewa kwa mkopo klabu ya OFK Beograd.

Aucho alijiunga na East Bengal ya India mwaka 2017 hadi 2018 na mwaka uliofuata akajiunga na Lel Makkasa ya Misri ambayo amemaliza mkataba nayo kabla ya kutua Yanga.

## TUNAJIANDAA...



Baadhi ya waamuzi waliochezesha mechi za Ligi Kuu Tanzania Bara msimu uliomalizika wakifanya mazoezi katika Uwanja wa Karume, Ilala jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# *Maguri akaribisha ofa akiikana Biashara Utd*

Na Adam Fungamwango

STRAIKA wa zamani wa Simba na FC Platinum ya Zimbabwe, Elius Maguri, amekanusha taarifa zinazovumishwa kuwa amejiunga na Biashara United, akidai ni mchezaji huru, mwenye uwezo wa kupokea ofa kutoka klabu yoyote inayomhitaji.

Maguri ambaye kwa sasa amemaliza mkataba wake na FC Platinum, amesema taarifa au tetesi zinazovumishwa, zinaweza kumsababishia kukosa timu, kwani kuna baadhi ya klabu zinaweza kuacha kumfuata wakidhani kuwa tayari amesaini kweli.

"Ukweli ni kwamba si kwamba sijasaini Biashara United tu, ila sijasaini timu yoyote ile. Kusema kweli hizi tetesi hata mimi nazisikia, zinaniweka kwenye wakati mgumu kwa sababu hivi sasa sina mkataba na timu yoyote, nasubiria ofa kwa klabu mbalimbali, hizi taarifa zinaniharibia. Mimi sina timu na naikaribisha timu yoyote ile kwa ajili ya mazungumzo," alisema Maguri.

Wakati Maguri akikanusha taarifa hizo, straika aliyezichezea klabu mbalimbali nchini, Atupele Green, amejiunga na klabu hiyo kwa mkataba wa mwaka mmoja.

Mtandao rasmi wa klabu ya Biashara United umetoa taarifa hiyo na kuweka picha ya mchezaji huyo akisaini.

Atupele ambaye ni zao la kikosi cha pili cha Yanga, amezichezea klabu mbalimbali za Ligi Kuu kwa kipindi tofauti kama Coastal Union, Kagera Sugar, JKT Ruvu ambayo kwa sasa ni JKT Tanzania, Singida United na Ndanda.

Biashara ambayo inajiwinda na michuano ya Kombe la Shirikisho na Ligi Kuu tayari imemsajili Tayo Odongo Mattew kutoka Zoo ya Kenya na ametia saini mkataba wa mwaka mmoja.

## Azam FC kucheza nyingi za kimataifa

Na Saada Akida

MTENDAJI Mkuu wa Azam FC, Abdulkarim Amin 'Popat', amesema wamejipanga vizuri kuhakikisha wanakuwa na mechi nyingi za ushindani za kirafiki za kimataifa kwa ajili ya maandalizi kuelekea michuano ya CAF ambayo inatarajiwa kuanza Septemba 10, mwaka huu ikiwa ni siku 19 kabla ya Ligi Kuu Bara kuanza.

Akizungumza na gazeti hili jijini Dar es Salaam jana, Popat alisema maamuzi hayo ya kutafuta mechi nyingi za kirafiki za ushindani ni baada ya kuona ratiba kuwa ngumu huku wakienda kushiriki michuano ya kimataifa wakati Ligi Kuu Tanzania Bara ikiwa haijaanza.

Alisema wamejipanga vizuri kutafuta mechi nyingi za ushindani za kirafiki ambazo zitasaidia timu yao kujiandaa na michuano ya kimataifa ambayo kwa muda mrefu hawakushiriki na kuhitaji kufanya vizuri.

"Tayari tumeshaingia kambini na kuanza mazoezi na ndani ya wiki hii kikosi kinatarajia kwenda nje ya nchini kwa ajili ya 'Pre Season' (maandalizi ya msimu mpya), itakayokuwa na mechi za kirafiki za ushindani kujiandaa na michuano hiyo," alisema Popat.

## Simbu: Mwiko kukata tamaa

Na Shufaa Lyimo

MWANARIADHA wa Tanzania, Alphonce Simbu, amesema anashukuru kuiwakilisha Tanzania katika mashindano ya marathon Olimpiki Tokyo, Japan na kumaliza nafasi ya saba jambo ambalo linampa hamasa ya kujipanga zaidi.

Katika mashindano hayo ambayo hufanyika kila baada ya miaka minne, Medali ya Dhahabu ilikwenda kwa Mkenya Eliud Kipchoge.

Akizungumza na gazeti hili jana, Simbu alisema licha ya kushika nafasi hiyo bado hajakata tamaa na badala yake ataendelea kujifua ili aweze kuongeza zaidi kiwango chake.

"Kwa sasa tunajiandaa kurudi nyumbani, tunashukuru tumemaliza salama kazi iliyotuleta huku, binafsi ninashukuru kwa nafasi niliyoipata japo kulikuwa na ushindani. Ninaomba Watanzania wasikate tamaa waendelee kutuunga mkono," alisema Simbu.

Hata hivyo, alisema amejifunza mambo mengi kutoka kwa wanariadha mbalimbali walioshiriki mashindano hayo na kwamba atakaporejea nchini atayafanyia kazi katika mazoezi yake.

# Michezo

Jumatano Agosti 11, 2021

Nipashe




Bayern kazi moja tu kumsajili Haaland UKURASA 22

KAMBINI...




Wachezaji wa Simba, Hassan Dilunga (kushoto) na Jonas Mkude wakielekea kupanda ndege katika Uwanja wa Julius Nyerere jijini Dar es Salaam tayari kwa safari ya Morocco, ambako klabu hiyo ilielekea huko jana tayari kwa kuweka kambi ya kujiandaa na msimu mpya wa Ligi Kuu na michuano ya kimataifa. **PICHA: SIMBA**

## Aucho atoa siri kutua Yanga SC

**Na Mwandishi Wetu**

BAADA ya kumwaga wino wa miaka miwili wa kuitumikia klabu ya Yanga, Kiungo mwili 'jumba' wa kimataifa wa Uganda, Khalid Aucho, amesema alichokifuata klabuni hapo ni mapenzi tu na si fedha.

Aucho ambaye alikuwa akihusishwa na Simba, Yanga na Azam FC, kabla ya kuamua kutua timu hiyo ya mtaa wa Twiga na Jangwani Dar es Salaam, amejiunga na miamba hiyo baada ya kumaliza mkataba wake na klabu ya Misr Lel Makkasa ya Misri.

Akizungumza na mwandishi wetu, Aucho alisema alikuwa na ofa nyingi mezani, lakini kwa namna Injinia Hersi Said (Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Usajili ya Yanga), alivyompigia simu na kuzungumza naye moja kwa moja kama familia, aliona klabu hiyo ni sehemu sahihi kwake.

"Sikutazama fedha bali ni kuhusu mapenzi ndiyo maana nimeamua kuichagua Yanga. Nimekuja Yanga kwa sababu ndiyo tuliyozungumza nao moja kwa moja na ninaona hapa ndipo ninaweza kucheza mpira. "Sikuzungumza na Simba, bali wao walikuwa wakizungumza na wakala wangu na hawakuweza kufikia makubaliano, ila mimi, nilizungumza moja kwa moja na injinia kama familia na ndicho kilinivutia zaidi nikaamua kuja Yanga," alisema Aucho.

Yanga inaendelea kukijenga kikosi chake kwa kusajili nyota mbalimbali kutoka ndani na nje ya nchi na Aucho anakuwa mchezaji wa tano kusajiliwa na kutambulishwa rasmi, wengine ni kipa raia wa Mali, Djigui Diarra kutoka Stade Malien ya kwao na washambuliaji Wakongo, Fiston Mayele kutoka AS Vita na Heritier Makambo(Horoya ya Guinea).

# Chama, Mukoko shida nyingine

## ●●● Wamorocco wazibomoa Simba, Yanga, waweka mzigo mrefu vigumu kuukataa, yumo pia Yacouba...

**Na Mwandishi Wetu**

WAKATI mabingwa wa nchi, Simba wakielekea Morocco jana kwenda kuweka kambi ya kujiandaa na msimu mpya huku watani zao, Yanga wakitarajiwa pia kuelekea nchini humo Jumatatu ijayo, Klabu za Morocco zimekuwa 'shida' kwa miamba hiyo ya Tanzania baada ya kupania kubomoa vikosi vya timu hizo.

**Simba na Yanga ambazo zitaiwakilisha nchi kwenye Ligi ya Mabingwa Afrika, zimeamua kuweka kambi nchini Morocco kujiandaa na msimu mpya wa Ligi Kuu pamoja na michuano hiyo ya kimataifa inayotarajiwa kuanza Septemba 10, mwaka huu ikiwa ni siku 19 kabla ya Ligi Kuu Bara kuanza.**

Tayari Yanga imethibitisha kufanya biashara na Klabu ya RS Berkane ya Morocco kwa kuiuzia winga wao Mkongomani Tuisila Kisinda, ambaye walimsajili msimu uliopita pamoja na kiungo mkabaji Mukoko Tonombe, wakitokea AS Vita ya kwao DR Congo.

Tuisila sasa atajiunga na Kocha wake wa zamani wa AS Vita, Florent Ibenge, ambaye Julai 5, mwaka jana alisaini mkataba wa miaka miwili wa kuinoa timu hiyo ya Ligi Kuu Morocco.

Hata hivyo, taarifa ambazo zimelifikia Nipashe na kuthibitishwa na viongozi wa timu hiyo ni kwamba kiungo mshambuliaji wa Simba, Mzambia Clatous Chama naye ana ofa nzito mezani kwa klabu yake pamoja na kiungo mkabaji wa Yanga, Mukoko pamoja na mshambuliaji Yacouba Songne wa miamba hiyo ya Jangwani.

Akizungumza na mwandishi wetu, Kaimu Ofisa Habari wa Simba, Ezekiel Kamwaga, alisema ni kweli kuna ofa kutoka Morocco kwa kiungo wao, Chama, ambayo wanaendelea kuijadili.

"Ni kweli kuna ofa ya Chama kutakiwa ipo mezani tunaijadili, na kuhusu Miquissone [Luis] suala lake la kutakiwa na Al Ahly bado, likikamilika tutawaeleza," alisema Kamwaga ambaye anakaimu nafasi hiyo iliyokuwa ikishikiliwa na Haji Manara aliyeachana na mabingwa hao wa Ligi Kuu na Kombe la FA.

Kwa mujibu wa vyanzo vyetu, klabu inayomhitaji Chama ni FAR Rabat ya Morocco, ambayo kwa sasa inanolewa na aliyekuwa Kocha Mkuu wa Simba, Mbelgiji Sven Vandenbroeck, na ofa iliyopo mezani kwa kiungo huyo ni dola 600,000 za Marekani sawa zaidi ya Sh. bilioni 1.3 za Tanzania.

Kwa upande wa Mukoko, Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Usajili ya Yanga na Mkurugenzi wa Uwekezaji wa Kampuni ya GSM ambao ni wadhamini wa klabu hiyo, Mhandisi Hersi Said, pia alikiri klabu hiyo kupokea ofa ya kiungo huyo raia wa DR Congo.

"Si Mukoko tu, pia kuna ofa ipo mezani ya Yacouba, tunazijadili tukiona zinafaa tutafanya biashara," alisema Hersi ambaye alihusika kwa zaidi ya asilimia 75 katika kufanikisha usajili wa wachezaji hao dirisha lililopita.

Mbali na wachezaji hao, pia Ibenge ameutaka uongozi wa RS Berkane kuhakikisha unamsajili mshambuliaji wa Simba, Mkongomani Chris Mugalu, aliyemaliza msimu wa Ligi Kuu Bara akiwa na mabao 15, moja nyuma ya kinara wa ufungaji, mchezaji mwenza wa timu hiyo, John Bocco.

Lakini pia kuna tetesi ambazo zinamhusisha kiungo mwingine wa Simba, Mzambia Rally Bwalya na klabu moja ya Morocco.


GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >